# Nipashe

Alhamisi Septemba 24, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580348

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Fatma Karume akwaa kigingi kingine, TLS yamtia hatiani

UKURASA 3


22 Nipashe

HABARI MICHEZO

DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA

TORREIRA CHAMBO YA PARTEY ARSENAL

••• Nii baada ya Atletico kumkataa Lacazette na kuonyesha nia kwa kiungo huyo, sasa Arteta...

ZISIKUPITE

UNITED KWA DEMBELE

DELE KUTUA PSG

MAX KUJIUNGA BARCA

MATTEO KUONDOKA ARSENAL

SANCHO KUBAKI DORTMUND

MILIK KUTUA NEWCASTLE

DAVIES ANUKIA SOUTHAMPTON

ARSENAL VITANI KWA AOUAR

ROMERO KUSEPA UNITED

RUDIGER NJIAPANDA CHELSEA

TAHA HATAKIWI LEICESTER

UPAMECANO AITESA UNITED

BREWSTER APOTEZEWA PALACE


EVERTON, ARIAS WATETA

UKURASA 22

# CHADEMA, ACT katika mtihani

• **Msajili** atoa onyo kali, wenyewe wafunguka...

*Endelea ukurasa 2*



MSAJILI WA VYAMA VYA SIASA, JAJI FRANCIS MUTUNGI

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MAHAKAMA YAKUBALI MSHTAKIWA KUTOKA GEREZANI KUHOJIWA POLISI**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imekubali ombi la Jamhuri kwamba Mkurugenzi wa Kampuni ya Jandu Constructions...









Kassim Majaliwa

## Kampeni kanyaga twende

• **CCM** waahidi matibabu bora...

*Ukurasa 2*

## Hadhari upepo mkali waja

UKURASA 3


**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

VOTE

Wasiliana nasi

Simu: 0686 101335,

Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Mjumbe wa Kamati Kuu, Kassim Majaliwa, akiweka shada la maua kwenye mnara wa kumbukumbu katika eneo la makaburi ilikozikwa miili ya watu waliofariki kwa ajali ya MV Nyerere, iliyotokea Septemba 20, 2018, katika kisiwa cha Ukara, Ukerewe mkoani Mwanza jana. **PICHA: OWM**

# CHADEMA, ACT kwenye mtihani

**Na Zainab Rashid, SJMC**

OFISI ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, imetoa onyo kwa vyama vya siasa kwa kukiuka masharti ya kisheria kipindi hiki cha kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Katika barua yake kuhusu hadhari hiyo, Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, kwa niaba ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, amewakumbusha wagombea wa vyama vya siasa kuzingatia masharti ya sheria katika kampeni hizo.

Kwa mujibu wa barua ya msajili huyo kwenda kwa makatibu wa vyama vyenye usajili wa kudumu iliyoandikwa Septemba 18, mwaka huu, vyama hivyo pia vimekumbushwa kufuata sheria katika kile kinachoitwa kuungana kwenye uchaguzi.

Alisema katika mikutano ya kampeni, baadhi ya wagombea wameonekana na kusikika wakiwaombea kura wagombea wa chama kingine cha siasa, akisisitiza kuwa sheria imeweka utaratibu wa vyama vya siasa kushirikiana katika uchaguzi.

"Vyama vya siasa kushirikiana bila kufuata utaratibu uliowekwa ni ukiukwaji wa sheria hiyo," alifafanua.

Alivikumbusha vyama hivyo kuwa wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa ni kuchukua hatua za kisheria dhidi ya chama cha siasa kinapokiuka Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Msajili wa Vyama vya Siasa hatasita kuchukua hatua stahiki za kisheria pale itakapothibitika chama cha siasa kimekiuka sheria hizo," alisema Nyahoza.

Ingawa Nyahoza hakutaja majina ya vyama vya siasa vilivyoingia katika hatari hiyo ya kukumbana na rungu lao, baadhi ya vyama vimeshaweka wazi kushirikiana na wagombea wa vyama vingine katika uchaguzi huo.

Mwanzoni mwa mwezi huu, mgombea urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, akiwa visiwani Zanzibar kuzindua kampeni kanda, alitangaza chama hicho kitamuunga mkono mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT- Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad.

Pia, hivi karibuni, Maalim Seif katika moja ya mikutano yake ya kampeni visiwani huko, alitangaza kuwa atamuunga mkono mgombea urais wa Tanzania Bara kwa tiketi ya CHADEMA, Lissu.

Juzi, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akihojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), alisema vyama hivyo viwili vimeshakubaliana na watatangaza utaratibu wa kushirikiano Oktoba 3, mwaka huu kwenye viwanya vya Mwembe Yanga jijini Dar es Salaam.

**TAFSIRI YA KISHERIA**

Alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia onyo la Msajili, Ofisa Habari wa ACT-Wazalendo, Naibu Katibu wa Uenezi, Habari na Uhusiano kwa Umma, Janeth Rithe, alisema ni vyema Ofisi ya Msajili ikasoma na kutafsiri vizuri sheria iliyoirejea katika taarifa yake kwa umma, akidai kuna tofauti kubwa kati ya ushirikiano na kuungana.

"Kuna suala la kuungana na kushirikiana. Kushirikiana ni kama ndoa ya kiserikali au kimila, kila mmoja anabaki na dini yake lakini ni wamoja na hiki ndicho tunachofanya. Kuungana ni kama ndoa ya kanisani, ikitaka wote kuwa dini moja na wamoja na hili ndiyo lililopo kwenye sheria ya msajili," alisema.

Rithe pia alishauri Ofisi ya Msajili kufuatilia vyama vingine vilivyotangaza ushirikiano mapema na havikuonywa, jambo ambalo alidai linazua maswali mengi.

"Tunamshauri Msajili atafute tafsiri sahihi ya sheria anayosimamia... tunaendelea na taratibu zetu kama tulivyopanga, tunajua sheria inasema nini na inataka nini, na tunajua kuna ushirikiano ambao vyama vinaweza kufanya bila kuathiri sheria na vikaendelea na kazi zao na hilo ndiyo tutakalofanya," alisisitiza.

Nipashe pia ilimtafuta Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, ambaye aliahidi kuwa leo atakutana na waandishi wa habari na kutoa kauli ya chama kuhusu barua hiyo ya onyo la Msajili kwa vyama vya siasa.

# Lissu aomba 'kura za kimbunga'

**Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amewaomba wananchi kumpigia kura nyingi ili apate ushindi wa kimbunga katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Lissu aliomba kura hizo jana alipokuwa kwenye mkutano wake wa kampeni eneo la Kamachumu wilayani Muleba mkoani Kagera, akiwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi kupiga kura siku hiyo, ili ushindi wa CHADEMA uwe wa kimbunga.

"Tukishinda kidogo, wataiba, tukishinda kawaida wataiba! Ili wasiibe, inabidi tushinde kwa kimbunga ili wakose kwa kuanzia, wakute kila kituo cha kuhesabia kura, katika jimbo, wilaya, mkoa tumeshinda," alisema.

Aliwataka wananchi wafanye kile alichokiita kurudisha mapigo kwa kuipigia kura CHADEMA, akitamba kuwa kwa kufanya hivyo, wapinzani wao watakuwa wamepigwa kwa namna ambayo hawatainuka tena.

"Mwezi ujao tuzuie hili balaa tupige kura tujikomboe, tarehe 28 mwezi Oktoba iwe ni siku mpya," Lissu alisema.

■ **Romana Mallya na Betrina Bishubo (SJMC)**

# Majaliwa aonya tozo kwa wajawazito, watoto

**Na Neema Emmanuel,** MAGU

MJUMBE wa Kamati Kuu ya CCM, Kassim Majaliwa, amewataka watendaji katika vituo vya afya, zahanati na hospitali za wilaya kuacha kuwatoza fedha wajawazito, watoto walio chini ya miaka mitano na wazee wanapohitaji huduma za afya.

Alitoa onyo hilo alipozungumza na wananchi wa vijiji vya Ilungu na Kisamba vilivyopo wilayani Magu akiwa njiani kuelekea jijini Mwanza.

"Tiba ya mama mjamzito, watoto, wazee, ni bure tumeleta fedha Sh. bilioni 10.8 kwanini watozwe hela wakati fedha zipo kama kuna mtendaji anayewatoza hao niliowataja wachukuliwe hatua kwa sababu ni wauaji pia tumewaboreshea vituo vya afya vyote ni vya kisasa, kuna sehemu ya kupima magonjwa yote, chumba cha upasuaji mdogo na mkubwa sambamba na chumba cha mama na mtoto," alisema Majaliwa.

Alisema, Magu bado kuna changamoto ya vituo vya afya, serikali itajenga vingine, ingawa imekamilisha vituo vya afya vya Kahangara, Lugeye na Kabila na kituo cha Kahangara.

"Endapo wananchi wa Magu wataichagua CCM, mkakati wa serikali ni kuhakikisha wilaya hiyo inapata maji ya uhakika.

Kwa upande wake, mgombea ubunge wa CCM katika Jimbo la Magu, Boniventure Kiswaga, alisema wananchi wa eneo hilo wamepata mafanikio mengi kwa kutatuliwa changamoto mbalimbali zilizokuwa zinawakabili.

HABARI KITAIFA

# Aliyerejeshwa na NEC Dar atamba ushindi bila kampeni

**Na Christina Mwakangale**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Ubungo kupitia CHADEMA, Boniface Jacob, amesema maisha yake kwa wananchi wa jimbo hilo, yanatosha kuchaguliwa kuwa mbunge, bila kutegemea kampeni.

Amesema pamoja na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kumrejesha kugombea kiti cha jimbo hilo, licha ya wagombea wa vyama vingine kuanza kufanya kampeni wiki tatu kabla yake, hata akifanya kampeni siku moja atachaguliwa na wananchi.

Boniface aliyasema hayo jana akizungumza na Nipashe kuelezea namna atavyoweza kufidia siku alizozuiwa kugombea, baada ya Agosti 29, mwaka huu, kupokea barua ya Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Ubungo, kumuengua kugombea ubunge jimbo hilo.

"Maisha yangu yenyewe tosha tu, ni kampeni hata ningezuiwa, ingeachwa siku moja, bado wananchi wa Ubungo wanahitaji tu kujua nagombea basi. Kwa hiyo 'issue' ya kampeni sio kitu," alisema.

Kwa siku nilizorudi tayari nimekamilisha mzunguko wa awamu ya kwanza, nilianza Mabibo, Makurumla, Manzese na Kimara, Sinza, leo (jana) namalizia Makuburi kata ya nane, leo (jana) naanza raundi ya pili," alisema Boniface.

Alisema wananchi wa jimbo hilo, wanafahamu utendaji kazi wake tangu akiwa diwani na hatimaye mbunge.

"Wakinichagua miradi niliyoianza tutaimalizia, vitu ambavyo nimefanya katika jimbo hilo kama shule, zahanati na barabara ni alama ambazo nimeziacha, kila kata nilizunguka na kushiriki kuleta maendeleo," alisema Boniface ambaye aliwahi kuwa meya wa Ubungo. Agosti 29, mwaka huu, katika ukurasa wake wa twitter, Boniface aliandika: Nimepokea barua kutoka kwa msimamizi wa uchaguzi Jimbo la Ubungo kuenguliwa kugombea ubunge."

Septemba, mwaka huu, NEC ilikubali rufani 13 na kuwarejesha katika orodha ya wagombea ubunge 13 baada ya kupitia nyaraka walizowasilisha.

Kati ya rufani hizo ni kutoka majimbo ya Singida Magharibi, Madaba, Ilemela, Namtumbo, Bagamoyo, Liwale, Tunduma, Bukene, Ubungo na Kigamboni.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Charles Mahera, ilisema kuwa Tume imechambua vielelezo, nyaraka na maelezo ya warufani na warufaniwa yaliyowasilishwa, ili kuhakikisha inatenda haki wa mujibu wa sheria.

# Hadhari upepo mkali waja

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa nchini (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa upepo mkali na mawimbi makubwa kwenye pwani ya Bahari ya Hindi katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

Aidha, imeeleza kuwa mvua zinazonyesha sasa kwenye baadhi ya maeneo ni za kawaida.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na TMA kupitia kwa mchambuzi wa hali ya hewa, Rose Senyagwa, kwa siku ya leo kunatarajia kuwapo upepo mkali unaofikia kilometa 40 kwa saa na mawimbi makubwa yanayofika mita mbili.

"Athari ambazo zinaweza kujitokeza ni ucheleweshwaji wa safari kwa vyombo vya baharini pamoja na shughuli za uvuvi nazo zitaathirika, hivyo ni vyema kwa watu kuchukua tahadhari," alisema Rose.

Alisema vipindi hivyo vya hali mbaya ya hewa si vya muda mrefu na wanategemea vitakuwa vipindi vifupi, na hali hiyo inaweza kukoma kesho.

Aidha, alisema TMA inaendelea kufuatilia hali ya hewa na itatoa taarifa kadri wawezavyo kwa wananchi ili kuchukua tahadhari kwa hali yoyote ya hewa itakayojitokeza.

Hivi karibuni TMA ilitoa utabiri wa msimu kwa mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka, na kuelezea hali ya mvua za chini ya wastani kutarajiwa, hivyo kusababisha ukame kwa baadhi ya mikoa.

Mikoa ambayo ilitajwa kutarajiwa kupata mvua chini ya wastani ni Dar es Salaam, Mwaza, Kagera, Shinyanga, Simiyu na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Kigoma, Kilimanjaro, Manyara, Arusha na Zanzibar.



Mgombea mwenza wa urais kupitia CHADEMA, Salum Mwalimu, akihutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Jimbo la Shinyanga Mjini juzi. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# Fatma Karume akwaa kigingi kingine, TLS yamtia hatiani

**Na Joseph Mwendapole**

KAMATI ya Maadili ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), imeondoa moja kwa moja jina la Fatma Karume katika orodha ya mawakili baada ya kumkuta na hatia ya kukiuka maadili ya uwakili.

Kwa uamuzi huo, Fatma mwenye namba ya uwakili 848 hataruhusiwa kufanya kazi za uwakili ndani ya mipaka ya Tanzania Bara mpaka itakavyoamriwa vinginevyo.

Baada ya uamuzi huo kutolewa mapema jana, Fatma ambaye ni mtoto wa Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume, aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter kwamba hatakata rufani kupinga uamuzi huo.

ALIVYOFUKUZWA KAMPUNI YA IMMA

Juzi Fatma aliandika kupitia ukurasa wake wa twitter kwamba amefukuzwa katika taasisi ambayo alisaidia kuijenga na kwamba dhambi yake ni uanaharakati.

Katika andiko hilo aliambatanisha barua kutoka kampuni ya IMMA iliyotiwa saini na wakili Sadock Magai ambaye ni Mshirika na Mwendeshaji wa taasisi hiyo ya uwakili.

Magai alithibitisha kuandika na kusaini barua hiyo ingawa alisema ilikuwa ni kwaajili ya mawasiliano ya ndani kwenda kwa fatma na haikutakiwa kwenda mitandaoni kama alivyofanya Fatma.

Barua ya kumfukuza kazi Fatma ambayo ilisambaa mitandaoni juzi uamuzi wa kumwondoa ulifikiwa Septemba 16, mwaka huu kupitia ushirikiano wao wa Equity Partners.

Kwenye barua hiyo, Magai alisema kikao kilijadili uhusiano uliopo baina ya fatma na washirika wenzake na kukubaliana kuwa hawahitaji tena kuendelea kuwa naye.

Fatma alisimamishwa uwakili mwaka mmoja Septemba 20, mwaka jana, Fatma alisimamishwa kufanya kazi za uwakili kwa mwaka mzima akishutumiwa kuishambulia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Sababu kubwa iliyotajwa kwenye shauri lake ni alichokizungumza katika kesi iliyofunguliwa na aliyekuwa Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mawasiliano wa chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu kupinga uteuzi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Adelarus Kilangi.

Prof. Kilangi aliteuliwa na Rais John Magufuli Februari Mosi, mwaka 2018.

Fatma Karume ni mwanasheria, wakili wa kujitegemea, mwanaharakati ambaye aliwahi kuwa Rais wa TLS katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2019.

Nipashe ilifanya jitihada za kumpata ili kujua hatua anazotarajia kuchukua, lakini simu yake ilikuwa ikiita muda wote bila kupokelewa.

# Mahakama yakubali mshtakiwa kutoka gerezani kuhojiwa polisi

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imekubali ombi la Jamhuri kwamba Mkurugenzi wa Kampuni ya Jandu Constructions and Plumber Ltd, Khairoon Jandu, kutoka gerezani na kwenda kuhojiwa na Jeshi la Polisi kwa siku tano.

Amri hiyo imetolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Kasian Matembele, baada ya upande wa Jamhuri kuomba kwenda kumuhoji mshtakiwa huyo.

Kabla ya amri hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, aliiomba mahakama kutoa kibali cha mshtakiwa Khairoon, kurejeshwa polisi kwa mahojiano kwenye kesi nyingine dhidi yake zilizopo kwenye hatua ya upelelezi.

"Mheshimwa tunaomba mshtakiwa arejeshwe polisi akahojiwe kwenye kesi zingine mbalimbali na hii, na atahojiwa kwa siku tano na kukabidhiwa tena mahakamani hapa Jumatatu Septemba 28, 2020," alisema Wankyo.

Mbali na Khairoon ambaye ni mke wa marehemu Jandu, washtakiwa wengine ni, Zainabu Tharia, binti yake, Wakili Mohamed Majaliwa na Meneja wa benki ya Stanbic, Ibrahim Sangawe. Katika kesi ya msingi inadaiwa, katika muda tofauti kati ya Januari na Juni, 2020 katika Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa wote kwa pamoja na kwa kudhamiria waliunda genge la uhalifu, kwa lengo la kughushi na kuiba fedha.

Katika shtaka la pili imedaiwa, Januari 16, 2017 jiji na Mkoa wa Dar es Salaam, washtakiwa Khairoon Jandu, Majaliwa na Sangawe, walighushi saini ya Inderjit Jandu katika nyaraka zilizoonesha kuwa ni halali za kikao cha Kampuni ya Jandu huku wakijua si kweli. Alidai katika kosa la tatu washtakiwa hao kasoro Zainabu, walighushi saini ya Inderjit Jandu katika nyaraka za kampuni zinazoonesha amechaguliwa kuwa Mkurugenzi wa kampuni hiyo akionyesha ni nyaraka halali huku akijua si kweli.

Washtakiwa hao pia wanadaiwa Mei 25, 2019 katika jiji na mkoa wa Dar es Salaam, wakiwa na nia ya udanganyifu walighushi saini ya I nderjit Jandu, wakionyesha kuwa amehamishia hisa za kampuni kwa Khairoon huku wakijua si kweli.

Shtaka jingine la kughushi linalomkabili Khairoon ni la nyaraka za wosia ulioandikwa na Inderjit akionyesha ni wosia halali huku akijua si kweli.

Ngukah aliendelea kudai kuwa katika shtaka la sita, saba na nane, Khairoon alitoa nyaraka za uongo kwa BRELA zilizoonyesha kuwa ni nyaraka halali za vikao vya kampuni ya Jandu kuwa amechaguliwa kuwa Mkurugenzi wa kampuni hiyo na pia amehamishiwa hisa za kampuni huku akijua kuwa si za kweli.

Katika shtaka la tisa washtakiwa wote wanadaiwa tarehe tofauti mwaka 2020 waliiba Sh. 1,033,860,100 mali ya Kampuni ya Jandu Constructions and Plumber.

Mshtakiwa Sangawe pia anadaiwa kati ya mwaka 2019 na 2020 akiwa ameajiriwa kama meneja wa benki ya Stanbic, alishindwa kutumia mbinu zote kuzuia wizi wa kiasi hicho cha fedha kilichokuwa kimehifadhiwa katika benki hiyo.

Katika kosa la mwisho la utakatishaji inadaiwa kati ya Januari 2019 na Juni 2020, jijini Dar es Salaam washtakiwa wote kwa pamoja walijipatia Sh. 1,033,860,100 mali ya Kampuni ya Jandu Construction huku wakijua kuwa fedha ni zao la kosa tangulizi la wizi.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani hapo kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na kwa mujibu wa upande wa mashtaka upelelezi wa shauri hilo bado haujakamili hivyo aliomba tarehe nyingine ha kutajwa.

Hakimu Matembele ameahirisha kesi hiyo hadi Septemba 28, 2020.



Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe (kushoto), akimnadi mgombea ubunge wa Tabora Mjini kupitia chama hicho, Msafiri Mtemelwa (kulia), kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Uyui, mjini Tabora juzi. **PICHA: SAID POWA**

# RC aagiza mabweni ya shule kufanyiwa ukaguzi

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, ameiagiza kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa huo, kufanya ukaguzi katika mabweni yote yaliyojengwa katika shule za msingi na sekondari kukabiliana na majanga ya moto.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akifanya ukaguzi wa vyumba vya madarasa na mabweni, yaliyojengwa kwenye shule za sekondari zilizopo wilayani Kalambo, mkoani humo.

Alisema kuwa kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa ndio yenye dhamana ya kufanya kazi hiyo, hivyo anaiagiza kutekeleza agizo hilo haraka iwezekanavyo, ili kuepukana na majanga ya moto, ambayo hutokea katika maeneo mengine nchini.

"Naiagiza kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa kuhakikisha inafanya ukaguzi wa miundombinu ya umeme katika mabweni ya shule zote hapa mkoani, kwani tatizo la majanga ya moto limeanza kuwa sugu katika maeneo mengine hapa nchini na kugharimu maisha ya wanafunzi, hivyo ni lazima mkoa uchukue tahadhari," alisema.

Naye Kaimu Ofisa Elimu wa Wilaya ya Kalambo, Mtinda Mwinuka, alisema amekwishatoa maelekezo kwa wakuu wa shule wilayani humo kuwa na utaratibu wa kufuatilia mienendo ya wanafunzi wao.

Alisema, baadhi ya wanafunzi ni watovu wa nidhamu na wanaoweza kutumia vifaa vya umeme vilivyopigwa marufuku kutumika bwenini na hivyo kuwa chanzo cha hitilafu za umeme na kuzua majanga na kusababisha vifo vya wanafunzi wenzao kwa ajali ya moto.

# Waziri afafanua urushaji matangazo vyombo vya kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imefafanua hatua yake ya kuvitaka vyombo vya habari vya kimataifa vinavyorusha matangazo yake kupitia vyombo vya habari vya Tanzania, imelenga kutambua vyombo wanavyoshirikiano navyo nchini.

Aidha, imesema lengo siyo kuvizuia kutangaza na kuendesha vipindi vyake nchini kama inavyoripotiwa.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, aliyasema hayo jana Jijini Dar es Salaam alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi mteule wa Uingereza nchini, Dk. David Concar.

Kwa mujibu wa Waziri huyo, vyombo vyote vya habari vya kimataifa zimeshatekeleza matakwa ya kisheria na kupata leseni ya kutangaza na kuendesha vipindi vyao.

Kuhusu suala la mabadiliko ya sheria za asasi za kiraia (NGOs) na vyama vya siasa, Prof. Kabudi alifafanua lengo lake ni kuongeza uwazi na uwajibikaji katika fedha zinazoingia kwa asasi hizo na matumizi yake.

Aidha, alisema linaendana na sheria na taratibu za kimataifa za kuzuia utakatishaji wa fedha na kuhakikisha makundi yenye nia ovu na misimamo mikali inayokwenda kinyume na tunu za demokrasia hayatumii njia hizo kupenyeza fedha zao.

Kwa upande wake, Balozi Concar, alisema mazungumzo yao mbali na kulenga masuala ya kidiplomasia na maendeleo, pia yalilenga kuangalia namna ya kuondoa malalamiko kutoka kwa baadhi ya NGOs na vyombo vya habari vya kimataifa kuhusu kile kinachodaiwa kuwa ni uminywaji wa haki ya uhuru wa vyombo vya habari.

Katika tukio jingine pia, Prof. Kabudi alikutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Denmark nchini, Balozi Mette Norgaard, ambapo mbali na suala la uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika nchini Oktoba 28,, wamejadili pia masuala yanayohusu ushirikiano katika sekta za elimu, afya, biashara na uwekezaji.

## HABARI KITAIFA

# Wananchi wafurahia vyeti RITA kusogezwa nyumbani

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wanaoishi Wilaya ya Temeke, mkoani Dar es Salaam, wamefurahia kusogezewa huduma ya cheti cha kuzaliwa karibu na makazi yao.

Akitoa taarifa hiyo, ofisa habari wa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA), Grace Kyasi, alisema tangu kuanza kwa kampeni ya 'One Stop Jawabu' ambayo imeanzishwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe, wananchi wengi wameonyesha mwitikio mkubwa wa kutembelea banda la RITA ili kusajili na kupata cheti cha kuzaliwa.

"Tunamshukuru sana Mkuu wa Wilaya hii ya Temeke, Godwin Gondwe kwa kuanzisha kampeni hii na kuzipatia fursa taasisi mbalimbali kushiriki ikiwamo RITA, ili kutoa huduma kwa wananchi papo hapo, jambo ambalo pia limeonekana kufurahishwa sana na wananchi wanaoishi maeneo hayo," alisema.

Baadhi ya wananchi waliofika katika banda la RITA kupata huduma ya cheti cha kuzaliwa, walishindwa kujizuia na kuelezea furaha yao.

Fatuma Seif, mkazi wa Mbagala Maji Matitu, alisema anaishukuru RITA kuwapelekea huduma nyumbani na kufanikiwa kusajili cheti cha mjukuu wake.

Said Mbonde, mkazi wa Mkuranga kwa upande wake alisema yeye na watoto wake walikuwa hawana vyeti vya kuzaliwa, lakini waliposikia Mkuu wa Wilaya anawaletea huduma hiyo nyumbani akaona umuhimu wa kwenda kuchukua cheti chake na familia yake kwa kuwa huduma nyingi zinahitaji cheti hicho hivyo itakuwa rahisi kuzipata.

Ofisa habari wa RITA, aliwasihi wananchi wazidi kujitokeza kwa wingi katika viwanja hivi vya Temeke Mwembe Yanga ili kusajili na kupata vyeti vya kuzaliwa katika banda la RITA kwa kuwa kampeni hiyo inahusisha wote ambao hawajawahi kuwa na vyeti vya kuzaliwa na waliozaliwa Tanzania Bara.

Kampeni ya 'One Stop Jawabu' ilianza rasmi Septemba 14 na inatarajiwa kuhitimishwa Septemba 28.




Wanafunzi wakipita kwa maandamano mbele ya Rais wa Zanzibar , Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani), wakati wa kilele cha miaka 56 ya Sherehe za Maadhimisho ya Elimu Bila Malipo katika uwanja wa Mao Dze Dong mjini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Maalim Seif aahidi kutunga sheria mpya gesi na mafuta

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kupitia Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema akipata ridhaa ya kuwaongoza wananchi, atatunga sheria mpya ya mafuta na gesi ambayo itakuwa na maslahi kwa Wazanzibari.

Katika mkutano wake wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka huu jana kwenye Viwanja vya Nyerere mjini Unguja, Maalim Seif alidai sheria ya sasa haileti faida kwa nchi, bali inawanufaisha watu wachache.

Alisema kampuni ya kimataifa ya Shell ina uwezo mkubwa wa kuchimba mafuta na wakati wa serikali ya umoja wa kitaifa akiwa Makamu wa Kwanza walikubaliana kampuni hiyo ifanye kazi ya uchimbaji mafuta, lakini anashangaa baada ya kuondoka serikalini makubaliano hayo hayakutekelezwa.

"Hakuna kisima cha mafuta kilichochimbwa kwa sababu wametafuta kampuni zisizo na uwezo," Maalim Seif alisema.

Mgombea huyo alisema kuwa akiwa Rais wa Zanzibar, atayarejesha makubaliano hayo ili kuwa na sheria ambayo inaiwezesha Zanzibar kuchimba mafuta na kuipa kazi kampuni ya Shell kuchimba mafuta.

"Ninataka hadi mwaka 2024, mafuta yawe yanachimbwa Zanzibar... mafuta ni yetu Wazanzibari. Kwa hiyo, kama mtanipa ridhaa, nitakwenda kuzungumza na wenzetu wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano mafuta kutolewa katika Muungano," aliahidi Maalim Seif.

Katika mkutano huo, Maalim Seif pia aliendelea kulaani tukio la wananchi watatu wa Kangagani, Pemba kushambuliwa kwa mapanga, akieleza kuwa ACT-Wazalendo haina sera ya kupiga watu.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Haji Duni, alidai kuwa ameanguliwa katika kugombea kinyang'anyiro cha kusaka uwakilishi wa Jimbo la Mtoni kwa sababu hajulikani jinsia yake.


# VACANCY ANNOUNCEMENT

We have been retained by our client, who is a leading college of **HEALTH AND ALLIED SCIENCES** in Dar-es-Salaam. We invite applications from suitable qualified and experienced Tanzanians to apply for the following vacant positions available in Dares Salaam. The college offers various NACTE approved Diploma Programmes.

**Vacant Positions**

1. Principal
2. Deputy Principal (Academic)
3. . Sr. Tutors, Tutors (Pharmacy, Nursing, Medical Lab Technology, Clinical Medicine and Physiotherapy)

**Principal**
**Qualifications:**

- Master's degree in Medicine; or Nursing or Pharmacy or Medical laboratory Sciences or relevant Paramedical Discipline.
- Minimum of 15 years administrative service in managing Health Sciences Colleges/Institutes.
- Good in communication and well versed with NACTE and HEALTH PROGRAMMES COUNCIL regulations.
- Proficiency in using ICT for education.

**Responsibilities**
**The Principal shall:**

(i) Facilitate learning (by teaching) of academic programmes in the institution;
(ii) Be the principal academic and administrative officer of a technical institution and Secretary to the Governing Board;
(iii) Be responsible to the Governing Board for the implementation of the decisions of the Governing Board;
(iv) Administrate the enforcement of by laws and regulations made by the Governing Board;
(v) Be responsible for formulation and implementation of policies to enhance the academic excellence of the institution;
(vi) Promote good relations with the Government and other organizations;

**Vice Principal- Academic**
People with similar Qualifications as above for principal but with less experience shall be considered.

**Sr. Tutors and Tutors**

- Minimum of Bachelor degree in the above-mentioned disciplines;
- Minimum of 3 years of experience in teaching
- Excellent communication skill in English and Kswahili.

**Remuneration:**
Remuneration will be the best in the industry and depend on the qualifications and experience;

**Mode of Application:**
Qualified candidates are encouraged to submit their applications accompanied with recent photograph, photocopies of certificates of degree awards, academic transcripts, curriculum vitae, birth certificate, experience certificates with names of three referees together with their contact addresses and any other relevant documents portraying their competences in the field.

Interviews for short listed applicants will be communicated to them.

***Apply on or before 10th of October 2020:***

**The Advertiser**
**P.O.Box no: 35745**
**Dar-es-salaam**
**Or mail to:**
**kiboshotz2020@gmail.com**

215914002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi wana kiu ya ilani ili wafanye maamuzi Oktoba 28

**KATIKA** vipindi vya moja ya runinga Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa alitoa onyo na maelekezo kwa wadau wa siasa katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Moja ya onyo alilolitoa ni vyama na wagombea wanaotumia lugha za kuudhi, matusi na kejeli ambazo zinavunja sheria na kushusha thamani ya utu wa mtu.

Msajili alikwenda mbali zaidi na kueleza matumizi ya maneno ya uongo, matusi ambavyo vina faini ya kati ya Sh. milioni 10 hadi 50. Licha ya kuwapo kwa uchaguzi mkuu, lugha ya matusi dhidi ya mtu mwingine hairuhusiwi na ni kosa kisheria.

Tunatambua kwa sasa kuna mpambano mkali baina vya vyama vinavyotaka kushika nafasi za udiwani, ubunge na urais, kila mmoja akipambana kwa namna anayoona inafaa kushawishi wapigakura kufanya maamuzi ifikapo Oktoba 28, mwaka huu.

Kama tulivyowahi kuvisihi vyama na wagombea kuwa lazima wasimame kwenye mstari kwa maana wakati huu ni wakati wa kueleza ukipewa nafasi ya kuongoza kwa nafasi yoyote utafanya nini ambacho kina manufaa kwa maisha ya mwananchi mmoja mmoja.

Kila chama kina ilani yake ambazo zimeeleza nini watafanya wakipewa nafasi kuanzia kwenye ilani yao ambayo imegusa maeneo mbalimbali.

Ni wakati wa vyama kuhakikisha wananchi wanapata ujumbe wa kilichopo kwenye ilani, kusoma mazingira na kujua mahitaji yao na kwa namna gani yanagusa maisha yao.

Tunatambua kabla ya kutengenezwa kwa ilani hizo ulifanyika utafiti wa kujua mahitaji ya wananchi na ndiyo vyama vingi vimeyaweka kwenye ilani zao na sasa wananadi sera hizo.

Inapotokea mgombea ameacha kupita njia hiyo ya kutumia vyema nyenzo yake na kuanza kuchanja mbuga kwenye maisha binafsi ya mgombea, udhalilishaji, kejeli na vijembe vyenye kudhalilisha utu wake moja kwa moja ameshindwa kusimamia na kutetea alichokiandaa kwenye ilani yake.

Na kama anashindwa kusimamia na kutetea alichokiandika ili kieleweke, kwa wananchi, maana yake anajipunguzia sifa za kuchaguliwa na hafai kuwa hata kiongozi wa mtaa wake.

Changamoto za wananchi kwenye maeneo yao ni kubwa na nyingi sana, na wapo ambao wanatamani zingetatuliwa, badala yake mgombea anajikita kuleza maisha binafsi ya mgombea mwingine.

Haitarajiwi kampeni zikatawaliwa na lugha za kuwagawa wananchi kwa kuwa labla walifanya maamuzi fulani huko nyuma ya kuchagua mtu wa chama fulani, ni lazima walikuwa na sababu za kufanya maamuzi hayo.

Kwa sasa ni uchaguzi mwingine ambao wananchi wana haki ya kuamua nani anafaa bila kushinikizwa kwa namna yoyote, zaidi ni kuwa na ilani ambayo inagusa matatizo ya wananchi.

Wagombea watambue Watanzania wa sasa si wa miaka ya 60, na wajue kuna teknolojia inayowawezesha kupata habari zote kwa haraka kupitia simu za mkononi, kwa hiyo wanawapima wagombea kuona ni kwa namna gani wanagusa maisha yao na si kuwadanganya ili kupata kura.

Kinachotakiwa kusikika kwenye majukwaa ya kisiasa ni kunadi sera na ilani za vyama, kufafanua kwa wananchi ili wafanye maamuzi sahihi Oktoba 28, mwaka huu, na si maisha binafsi, matusi na kejeli.

Tunaamini wapigakura wana uwezo wa kuchambua, kuchuja mambo wanayoelezwa, hivyo tunasisitiza kuwa wagombea na vyama vyao waeleze mambo yao yaliyomo kwenye ilani, ambazo zinaeleza nini wanapanga kufanya, mikakati na mengineyo katika kuwaletea maendeleo wananchi na taifa kwa ujumla.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kasi inahitajika kuhudumia afya za wazee nchini kote

**MZEE** ni nani? Nadhani si jambo lisilohitaji ufafanuzi, kwani kila mmoja anaielewa fika, kwa kila mmoja kama asipoushuhudia kushoto, basi uko kulia ndani ya jamii.

Kwa tafsiri ya kiufafanuzi, uzee na kuzeekani hatua ya mwisho ya makuzi ya binadamu, ambayo mchakato wake unaanzia utoto, ikifuatiwa na ujana. Sifa kuu ya mzee, huwa anapungukiwa nguvu za kufanya kazi, kuliganisha na alikotoka ujanani.

Mtu anapofikia hatua hiyo ya umri mkubwa, uwezo wa kumudu gharama za maisha unapungua. Hapo inahusu pia kugharimia afya, hivyo kubaki kuwa wa kusaidiwa na watoto familia na jamii kwa ujumla.

Kwa bahati nzuri nchini mamlaka ya kiutawala umeshaliona hilo. Watu waliofikisha umri wa miaka 60 na zaidi wanapaswa kisheria kupata huduma za afya bila ya malipo, katika vituo vyote vya afya vya serikali, ili kuboresha afya zao, waendelee kuishi muda mrefu.

Hiyo ni kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, inayoelezea kwa kina sababu za kuwapo kwake, kutokana na uzoefu wa mazingira hali, kusimamia mwongozo wa utoaji huduma za afya.

Sera ya Taifa ya Wazee, inawatambua kuwa rasilimali muhimu katika maendeleo ya taifa, kwa kuwashirikisha katika uamuzi muhimu unaowahusu kwa ujumla wao.

Suala la kushirikisha jamii hiyo katika uzalishaji mali, kufikia hatua ya kuondoa umaskini miongoni mwao na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wazee, kutoa ulinzi wa kisheria katika sura ya wao ni kundi maalum.

**Vilevile, inalenga kuwaelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni, kwa kuwa kila mmoja ni mzee mtarajiwa, pindi atakapojakiwa kufika huko.**

Vilevile, inalenga kuwaelimisha vijana kuhusu masuala ya uzee na kuzeeka na kuwajengea uwezo wa kufanya maandalizi ya maisha kuelekea uzeeni, kwa kuwa kila mmoja ni mzee mtarajiwa, pindi atakapojakiwa kufika huko.

Ndani ya Sera ya Taifa ya Wazee, serikali inaweka wazi kuwatambua wazee kwamba ni rasilimali na hazina kubwa katika maendeleo ya nchi hii.

Aidha, inataja nchi kuwa kielelezo tosha cha mchango mkubwa wa wazee walioutoa katika nyanja kama za kisiasa, kiuchumi, kijamii na utamaduni.

Sababu hizo na nyingine nyingi za kutambua umuhimu wa wazee, ndio zimezaa sera hiyo, ili wazee wapate huduma za afya bure kwenye vituo vya afya vya serikali.

Ingawa kuna changamoto mbalimbali katika utoaji huduma za afya kwa wazee, ni vyema kukiri uwapo wa juhudi zilizofanyika, zikiwamo kuwapa vitambulisho vinavyowawezesha kupata huduma hiyo bure.

Ndani ya hayo yaliyo chanya, kuna viashiria vya sehemu ya upungufu kama kukosekama dawa katika vituo vya afya, huku wakielekezwa na baadhi ya wahudumu wa afya kuwa wakanunue katika maduka ya dawa.

Mtazamo na mkakati ulioko kiserikali, ni kuongeza idadi ya wazee waliopatiwa vitambulisho vya kuwawezesha kupata matibabu bure, kutoka 213,025 katika miaka mitano iliyopita hadi 1,042,403 wa leo hii.

Pia, kiuna maengine mengi kama vile kuingeza makazi yanayomilikiwa na serikali kufikia 16 na kuimarisha upatikanaji huduma za afya kwa wazee hao.+

HABARI KITAIFA

# TAKUKURU yapokea malalamiko 100 kila siku

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana Rushwa nchini (TAKUKURU), imesema kila siku inapokea zaidi ya malalamiko 100 ya rushwa nchini.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema malalamiko hayo ni pamoja na wananchi kudhulumiwa fedha kupitia mikopo umiza (yenye riba kubwa) na wadaiwa sugu waliodhulumu fedha za wakulima.

Alisema TAKUKURU imekuwa ikitatua kero hizo ili wananchi wawe salama na mali zao, huku akiwataka kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa.

“Kuna taarifa mitandaoni kuwa tunawabambikizia watu kesi halafu tunataifisha fedha za watuhumiwa hao kutoka katika akaunti zao za benki jambo ambalo si kweli,” alisema.

Alisema taasisi hiyo inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007.

“Napenda wananchi wafahamu TAKUKURU inapokuwa imepokea tuhuma inafanya uchunguzi ili kupata ushahidi wa tuhuma hizo na baada ya kukamilisha upatikanaji wa ushahidi huo jalada la uchunguzi linapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma (DPP),” alisema.

Alisema jalada hilo hupelekwa kwa DPP kwa ajili ya mapitio ya ushahidi waliokusanya na akijiridhisha na ushahidi ndipo kesi hufunguliwa mahakamani.

Akizungumzia kuhusu uchaguzi mkuu, alisema TAKUKURU inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi namba 1 ya mwaka 1985 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Namba 6 ya mwaka 2010 na kuwataka wananchi kutojihusisha na rushwa wakati wa uchaguzi.



Mafundi wakiendelea na maandalizi ya kujenga makutano ya barabara za Mawasiliano na Sam Nujoma kwa kiwango cha zege, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Hasunga atoa neno utengenezaji tela trekta

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ameipongeza kampuni ya usambazaji zana za kilimo ya Agricom Africa, kwa kutumia vijana wa Tanzania kutengeneza matela ya trekta kwa gharama nafuu ukilinganisha na zile za kuagiza nje.

Akizungumza katika hafla ya utilianaji saini mkataba kati ya Benki ya CRDB na kampuni tatu za usambazaji wa zana za kilimo jana, Waziri Hasunga alisema Agricom Africa imekuwa ikitekeleza kwa vitendo azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda kwa kuwaamini vijana na kuwatumia kufanya uzalishaji.

“Kilimo ni sekta muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda na pia kilimo kimekuwa kinatoa mchango wa asilimia 28 ya pato la taifa. Naipongeza sana Agricom Africa kwa kuona hilo na kuanzisha teknolojia ya utengenezaji wa matela ya trekta hapa nchini,” alisema Hasunga.

Alisema teknolojia hiyo pia itachangia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto ya ajira kwa vijana wa Tanzania pamoja na kukuza uchumi wa wananchi kwa ujumla.

Mkurugenzi Mtendaji wa Agricom Africa, Angelina Ngalula, alisema wataendelea kutumia fursa zilizopo kuhakikisha sekta za viwanda na kilimo zinaongeza tija katika uchumi wa Taifa kwa kuwafanya wakulima nchini waendeshe kilimo cha kisasa.

“Tunaishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuweka mazingira rafiki kwa watu wa sekta binafsi, kuwekeza katika miradi mbalimbali. Tutatumia mazingira hayo kuhakikisha tunatoa mchango stahiki, ili kufikia malengo ya nchi iliyojiwekea,” alisema Ngalula.

# Wavuvi walia bei ‘kiduchu’ ya sangara

**Na Richard Makore,**
MWANZA

CHAMA cha Wavuvi nchini (FUO), kimeiomba serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha sera za biashara ili samaki aina ya sangara wanaouzwa viwandani waweze kuwanufaisha.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Mwenyekiti Mtendaji wa chama hicho, Juvenary Matagili, alisema wavuvi wanauza samaki mzima viwanda, lakini wao wanamchambua na kutoa bidhaa zingine zenye thamani yakiwamo mabondo.

Alitoa mfano katika mchanganuo huo, wenye viwanda wanapata steki ya samaki, mabondo, mafuta, mifupa pamoja na magamba, lakini mvuvi anapata bei ya samaki akiwa mzima.

Aliongeza kwamba wavuvi wanahitaji kuuza samaki akiwa ametenganishwa ama kupewa bei zaidi kwa wasindikaji ambao ni wanamiliki wa viwanda.

Aliongeza kuwa bei ya mabondo ya juu kuliko minofu ya samaki, lakini wavuvi wanapewa bei kidogo kwa samaki ambaye hajatenganishwa.

Alisisitiza kuwa ikiwa samaki hao hawatauzwa wakiwa wametenganishwa wavuvi wataendelea kunyonywa, huku akiomba serikali kuwasikiliza ili waweze kunufaika.

## Taarifa kiganjani yawafikia wengi NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

TEKNOLOJIA ya kisasa ya taarifa kiganjani inayotumiwa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), kuwafikia wateja imewafurahisha wanachama wa shirika hilo, waliotembelea maonyesho ya madini yanayoendelea mkoani Geita.

Baadhi ya wananchi hao, waliofika katika banda la NSSF katika viwanja vya Bombambili, ambako maonyesho hayo yanafanyika, walishukuru shirika kwa kurahisha upatikanaji wa taarifa za wanachama kwa njia ya simu ya kiganjani au mtandaoni.

Christian Lazaro, mkazi wa Geita, mmoja wa wananchi aliyetembelea banda la NSSF, alisema kuwa amepata elimu nzuri juu ya hifadhi ya jamii na kuelewa namna ya kupata taarifa zake za michango na nyingine mbalimbali kwa kutumia simu, bila ya kufika ofisi za NSSF.

“Nimejaribu kuuliza kwenye simu yangu nimepata taarifa zote kuanzia nilipoanza kuchangia. Napenda kuwashukuru NSSF kwa kuleta njia ya kisasa ya kupata taarifa kwa kutumia simu ya kiganganjani, taarifa zako zote unapata kiganganjani,” alisema Lazaro.

“Ukiona mwajiri apeleki michango basi jaribu kufuatilia mapema, ili unapofika umri wa kustaafu uwe na uhakika kuwa michango yako ilienda yote na usisumbuke,” alisema.

Meneja wa Afya, Usalama na Mafunzo katika mgodi wa GGM Geita, Dk. Kiva Mvungi, naye alifurahishwa na mfumo huo wa kupata taarifa kupitia simu ya kiganjani.

“Nimeona programu mpya ya kuangalia taarifa za mwanachama kwenye simu ya mkononi, kama vile kuangalia salio la michango yangu. Katika mwendelezo wa mambo mazuri ambayo NSSF wameleta ni pamoja na hii programu, baada ya kuonyeshwa programu hiyo hapa kwenye banda la NSSF nimeona michango yangu, pia salio langu,” alieleza.

Naye mkazi wa Geita, Franklin Kabumbire, ambaye ni mwanachama wa NSSF, alishukuru NSSF kwa kumuhudumia vizuri katika kumpatia mafao yake.

# RC Mongela apokea miradi ya bil. 8/-

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, amepokea mabomba ya maji kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji 22 katika wilaya tano, yenye thamani ya Sh. bilioni 8.3.

Akizungumza wakati akipokea mabomba hayo, alisema miradi hiyo ikikamilika inatarajia kuhudumia watu 120,000, hivyo watendaji wa halmashauri na RUWASA wanapaswa kusimamia kikamilifu, ili ikamilike kwa wakati.

"Kama mnavyojua kwenye miradi ya maji tumepata takribani Sh. bilioni 8.3 kama mkoa, kwa ajili ya miradi 22 yenye urefu wa takribani kilomita 238, pamoja na hiyo tumepokea karibu Sh. milioni 900, kwa ajili ya kujenga uwezo wa vyombo vya usimamizi wa maji, tunategemea itahudumia watu takribani 120,000 pindi utakapokamilika," alisema Mongella.

Alisema, miradi hiyo iliasisiwa na Rais John Magufuli na utekelezaji unafanyika lengo kubwa ni kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama, hasa maeneo ya vijijini.

Kwa upande wake Meneja RUWASA Mkoa wa Mwanza, Immaculata Emmanuel, alisema wanatekeleza miradi hiyo 22 kwenye wilaya tano, sawa na halmashauri sita ikiwamo ya Magu, Kwimba, Sengerema na Buchosa, Misungwi na Kwimba pamoja na Ukerewe huku Wilaya za Ilemela na Nyamagana hazipo kwenye mpango huo kwa vile zinasimama na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA).



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), Mark Ocitti (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana wakati kampuni hiyo ilipotangaza ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo nchini ikiwa ni awamu ya pili. Habari Uk. 9. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kongwa yapania kuwa kijani kwa mikorosho

**Na Ashton Balaigwa,** KONGWA

SERIKALI wilayani Kongwa, mkoani Dodoma imedhamiria kupunguza ukame na athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa kuifanya wilaya hiyo kuwa ya kijani kwa kupanda miti mingi ya mikorosho, ambayo pia itasaidia kukuza uchumi wa wananchi wilayani humo.

Kwa kuanzia, wilaya hiyo imeshapanda miti ya mikorosho 306,886, ambayo sawa na ekari 10,229.5 na imeanza kupunguza tatizo la ukame linaloikabili wilaya hiyo. Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Suleiman Serera, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya kilimo cha korosho kwa maofisa ugani na wakulima wa zao hilo, yanayotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele. Mkuu huyo wa wilaya alisema, ili kufikia malengo hayo, wameanzisha mkakati wa kila kaya kuwa na ekari moja ya zao la korosho katika jumla ya kaya 74,000 zilizopo katika wilaya hiyo na tayari uhamasishaji umeshaanza kufanywa kwa wataalamu wa kilimo na viongozi wa serikali kupita nyumba hadi nyumba kutoa elimu.

"Wilaya yetu ina tatizo la ukame, tumekubaliana na Wakala wa Misitu tupande miti mbalimbali ya mazao na matunda ikiwamo mikorosho na tayari imeshapandwa na tumeona mafanikio na ukame umeanza kupungua," alisema.

Ofisa Kilimo, Ushirika na Umwagiliaji, Jackos Shija, alisema kuwa tayari wameshaagiza miche 2,220,000 ya mikorosho kutoka TARI Naliendele, kwa ajili ya kuzipatia kaya hizo zianze kupanda zao hilo na kutokana na umuhimu wake wa kurejesha uoto hali ya asili.

Shija alisema pia mkakati ni kulifanya zao hilo kuwa la kudumu na la kibiashara, ambalo litaongeza kipato cha mkulima na kuifanya wilaya hiyo sasa kukua kiuchumi.

Naye Mratibu wa Kitaifa wa zao la korosho kutoka TARI Naliendele, Dk. Geradina Mzena, alisema mkakati uliopo wa serikali ni kulifanya zao hilo hapa nchini kuzalishwa kwa wingi katika mikoa yenye fursa, ikiwamo Mkoa wa Dodoma na wilaya zake kwa kuwa mahitaji ya korosho ni makubwa katika nchi za Ulaya.

# Wakulima watahadharishwa dawa za kuua wadudu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara mkoani Shinyanga wametakiwa kuacha kutumia dawa zinazotumika kuua wadudu wanaoshambulia pamba na tumbaku kwenye mazao ya nafaka ili kulinda afya ya mtumiaji hasa kwa wajawazito na watoto.

Ofisa lishe mtafiti, elimu na mafunzo lishe, Neema Joshua, kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe, alisema hayo jana wakati wa mafunzo ya umuhimu wa lishe katika kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa kwa waandishi wa habari wa mkoani Shinyanga.

Alisema mkulima anapotumia viuatilifu kwenye zao la pamba na tumbaku, mazao ya kibiashara na chakula kunasababisha kutengenezwa kwa sumbukuvu ambayo inaathiri mtumiaji na mtoto aliye tumboni.

Kwa upande wake, mratibu wa chakula na lishe mkoani Shinyanga, Denisi Madeleke, alisema tatizo la upungufu wa damu kwa kinamama walio katika umri wa kuzaa (15-49), katika mkoa wa Shinyanga ni asilimia 30 kwa mwaka 2018 na awali tatizo hilo lilikuwa asilimia 59.4.

# Mgombea atangaza neema huduma za jamii

**Na Happy Severine,** SIMIYU

MGOMBEA ubunge Jimbo la Bariadi mkoani Simiyu kupitia CCM, Andrew Kundo, ameahidi kutatua changamoto ya huduma za afya, barabara, maji na elimu kwa wananchi wa kata ya Ikungulyabashashi na Gudui.

Mhandisi Kundo alisema kuwa endapo atachaguliwa kuwa mbunge wa jimbo hilo, atashughulikia kero hiyo ili wananchi waweze kuishi vizuri.

Alitoa ahadi hiyo kwenye mkutano wa hadhara wa kampeni katika jimbo hilo.

Katika Shule ya Msingi ya Mwahalaja, mgombea huyo aliahidi kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ambavyo vinahitaji zaidi ya mabati 100.

Katika mkutano huo, Kundo alimwombea kura mgombea wa urais kupitia CCM, John Magufuli.

## HABARI KITAIFA




Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Richard Kwitega (katikati), akiwa pamoja na Mkurugenzi Mtendaji Mkuu wa Benki ya NCBA Tanzania Ltd, Margaret Karume (kulia), na Mkurugenzi wa Biashara na Huduma za Kidigitali wa benki hiyo, Gift Shoko, baada ya matembezi yaliyoendana na uzinduzi wa matawi mawili mapya ya benki hiyo ya Clock Tower katika jengo la TFA, na Sokoine Central Plaza, jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 30 wa kilimo wapata ufadhili

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni mwendelezo wa kusaidia sekta ya kilimo nchini, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) imetangaza kuwa itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 30 wa kilimo katika mwaka huu wa fedha (2020/2021).

Idadi hiyo itafanya jumla ya wanafunzi ambao tayari wameshanufaika na mpango huo wa ufadhili wa masomo kufikia 70 baada ya SBL kutoa ufadhili kwa wanafunzi 40 mwaka wa fedha 2019/2020.

Waliobahatika kupata ufadhili huo kwa sasa wapo vyuoni wakiendelea na masomo. Ufadhili huu hutolewa na kampuni ya SBL chini ya mpango unaojulikana kama 'Kilimo-Viwanda Scholarship Program'.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili wa mpango huo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema mpango wa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo unalenga kuisaidia serikali kuwajengea uwezo wa kuzalisha zaidi wakulima kupitia kuwafundisha wataalamu wa kilimo ambao watawasaidia na kuwashauri.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa, SBL imetenga jumla ya Sh. milioni 120 ambazo zitatumika kila mwaka kwa ajili kuwalipia wanafunzi wenye sifa na ambao lengo lao ni kusoma masomo ya kilimo na kuongeza kuwa wanufaika watatoka katika familia za wakulima zenye kipato cha chini.

"Ili kutekeleza mpango huu tunashirikiana na vyuo vinne vya ndani ambavyo vinafundisha masomo ya kilimo. Tunaamini mpango huu utasaidia kuongeza idadi ya wataalamu wa kilimo hapa nchini ambao ni nguzo muhimu ya kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wao na mwisho wa vipato vyao," alisema.

Alisema vyuo ambavyo kampuni hiyo inashirikiana navyo katika utekelezaji wa programu hiyo ni Kaole Wazazi College of Agriculture kilichopo Bagamoyo mkoani Pwani, Kilacha Agriculture and Livestock Training Center kilichopo Moshi, Mt. Maria Goretti College of Agriculture cha Iringa pamoja na Igabiro Training Institute of Agriculture kilichopo Bukoba, mkoani Kagera.

Akitoa neno la shukrani kwa niaba ya wakuu wenzake wa vyuo vinavyonufaika na mpango huo, Mkuu wa Chuo cha Kilacha Agriculture and Livestock Training Center, Benito Mwenda, aliishukuru SBL kwa kuja na wazo la kutoa ufadhili wa masomo ya kilimo na kuongeza kuwa ili kilimo kiweze kuwa chenye tijawataalamu wengi wanahitajika.

"Tunayo furaha kwa kuwa ufadhili huu unawalenga wanafunzi wanaotokea katika familia zenye vipato duni ambao kama siyo msaada wa SBL, wasingeweza kupata fursa ya kusoma na kubadilisha maisha yao pamoja na ya jamii zao," alisema.

# Utafiti wa miti kuchochea ukuaji uchumi

**Na Daniel Sabuni,** MOROGORO

TAASISI ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI), imesema utafiti na utambuzi wa majina ya miti na aina zake utasaidia kuchochea kasi ya uchumi wa kati uliopo sasa pamoja na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti wa uzalishaji misitu wa TAFORI, Dk. Siima Bakengesa, aliyazungumza hayo jana ofisini kwake nje kidogo ya mji wa Morogoro na kuongeza kuwa misitu ni utajiri na ajira kwa wingi. Alisema utafiti na utambuzi wa aina ya miti ni jambo la muhimu kwa mendeleo ya kiuchumi ya Tanzania yenye uchumi wa kati unaotegemea viwanda kwani kufanya hivyo wanajua miti inayofaa kupata mbao kwa ajili ya kuezeka nyumba.

Pia, itasaidia kutambua inayofaa kwa ajili ya samani, dawa za asili na pia kuleta hali ya hewa nzuri na kutengeneza vyanzo vya maji na viwanda vya mbao kwa ujumla wake.

"Tuna zaidi ya sampuli 5,000 za miti kwenye sehemu maalumu za kuhifadhia na kupimia (Herbarium). Tumeshatafiti na kujua majina yake ya kiasili kwa kila kabila na ya kisayansi (kilatin), hii inatusaidia kutambua miti yenye umuhimu zaidi katika uchumi wa viwanda kama mvule, mkongo, mtiki, mpingo na mikoko, pamoja na miti ya kufaa kwenye vyanzo vya maji, dawa na vivuli," alisema Bakengesa.

Alisema watu wengi hukata tamaa ya kuanzisha mashamba ya miti kibiashara kwa madai ya kuwa miti huchukua muda mrefu hadi kuvunwa na kwamba uharaka wa kukua kwa miti unategemea vitu vingi ukiwapo aina ya udongo, hali ya hewa, ubora wa vipandio, lakini kinga dhidi ya magonjwa na wadudu waharibifu.

Kwa mujibu wa sensa ya miti ya mwaka 2015, sehemu ya nchi yenye miti ni takribani asilimia 50 kwa kuwa na idadi inayokadiriwa kuwa hekta milioni 48 zenye miti na familia 261.

Dk. Bakengesa alitoa mfano wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Iringa, Njombe na Mbeya kuwa yana maeneo yaliyopandwa miti ya biashara kiasi cha hekta 429,539, Kanda ya Ziwa yenye mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Geita.

Pia hekta 65,734, Kaskazini; Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara, hekta 34,322, Kanda ya Mashariki: Morogoro, Dar es Salaam, Pwani, hekta 12,450, Kanda ya Kati yenye mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora hekta 6,969 na Kanda ya Magharibi yenye mikoa ya Kigoma hekta 8,105, hivyo kanda zote saba kuwa na hekta 554,500 za miti.

# TBS yatatua matatizo Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limetatua matatizo mbalimbali yanayowakabili wananchi jijini Dar es Salaam kupitia maonyesho ya One Stop Jawabu yaliyoanza Septemba 14, mwaka huu, katika Viwanja vya Mbagala Zakhiem.

Maonyesho ambayo yamepewa jina la One Stop Jawabu yameandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe kwa lengo la kusogeza huduma mbalimbali kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuzipatia ufumbuzi.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo jana kwenye Viwanja vya Mwembe Yanga, Ofisa Uthibiti Ubora wa TBS, Eugenia Kibasa, alisema kupitia maonyesho hayo wanahudumia wananchi mbalimbali wa Wilaya ya Temeke ambao wanafika wakitaka kujua masuala yanayohusu usajili wa majengo yao ya biashara.

Aliwataja wengine ni wenye maduka ya vyakula, maduka ya kuuza vipodozi na 'supermarket' kubwa na za kati.

Aliongeza kuwa wananchi hao wanapatiwa elimu kuhusu bidhaa ambazo wanaagiza kutoka nje ya nchi, kwani wanatakiwa wawe wameomba usajili wa hizo bidhaa kabla ya kuziingiza nchini.

"Pia tunawaelekeza wananchi kuhusiana na usajili wa bidhaa zile zinazozalishwa nchini tunajua kwamba kuna wajasiriamali ambao ili wapate leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS wanatakiwa wapitie SIDO ambao ndiyo wanaowathibitisha kwamba wao ni wajasiriamali wadogo," alisema Kibasa.

# Maadili shuleni yaepusha mimba

**Na Yasmine Protace**

UONGOZI wa Shule ya Sekondari St. Mark's iliyopo Kongowe jijini Dar es Salaam, umesema kuwajenga kimaadili wanafunzi wao kwa takribani miaka 17 ya kuanzishwa kwake, hakuna mtoto aliyeacha shule kwa kupata ujauzito.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa shule hiyo, Peter Mutembei, katika mahafari ya 17 ya kidato cha nne.

Alisema maadili yanapoanza kutolewa shule yanawajenga kiuwezo watoto na kutojishughulisha na mambo yasiyofaa.

"Walimu ni walezi wakubwa wa watoto na wanakuwa nao karibu na kushinda nao muda mrefu shuleni, pia walimu wanafahamu zaidi tabia za wanafunzi, hivyo wanalazimika kuwapatia maadili ili wote wawe kitu kimoja," alisema.

Alisema hayo yote ni maadili ambayo yanatolewa kwa wanafunzi wao na wamekuwa wakiwasisitiza hata wakirudi nyumbani wayaendeleze maadili hayo.

Mkuu wa shule hiyo, Leticia Joseph, aliipongeza kwa kuandaa utaratibu

## Vikwazo utekelezaji sera ya uwekezaji vyaanikwa

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema licha ya kuwapo kwa utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji ya Mwaka 1996 na sera mbalimbali za kisekta kuhusu uwekezaji, bado kuna changamoto zinaikabili ikiwamo uratibu wa masuala ya uwekezaji, utangazaji wa fursa na uwezeshaji wa uwekezaji nchini.

Hayo yalielezwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Dorothy Mwaluko, katika hotuba yake ya ufunguzi iliyosomwa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uwekezaji, Aristides Mbwasi, juzi jijini Dar Salaam katika mkutano wa wadau wa sekta binafsi wa kupitia rasimu ya taarifa ya tathmini ya uwekezaji ya mwaka 1996.

Lengo la mkutano huo ni kutoa fursa kwa wadau wa sekta sekta binafsi kupitia na kutoa maoni yao kuhusu rasimu ya taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996.

Alisema wameanzisha rasimu hiyo kwa sababu kila nchi inafanya jitihada za kuvutia wawekezaji kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji, ili kulinda na kukuza uchumi wa nchi zao kwa kuvutia teknolojia bora, mitaji, fedha za kigeni na kuongeza ajira katika mataifa yao.

"Katika kipindi hiki ambacho tumeingia kwenye soko la pamoja la Afrika Mashariki (EAC), soko la Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), na majadiliano ya kuingia katika soko huru la biashara na mauzo Afrika, tunahitaji kuwa na sera madhubuti za kuvutia na kuwezesha uwekezaji katika sekta mbalimbali ili kutumia vilivyo fursa zitokanazo na jumuiya hizi," alisema Mwaluko.

Alisema katika Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya mwaka 1996, imebainisha malengo mahsusi sita na malengo nane ya kisekta ambayo ni kuhamasisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya nje; kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi; kuhimiza na kuvutia matumizi ya teknolojia za kisasa katika uwekezaji na kuweka mfumo mzuri na wa wazi wa kisheria.

Mwaluko alisema pia ni kuondoa urasimu katika taratibu za upatikanaji wa vibali vya uwekezaji na kwamba sera hiyo inatoa mwongozo wa uwekezaji katika sekta mbalimbali za uchumi zikiwamo sekta za viwanda, utalii, usafirishaji, kilimo na madini.

Kadhalika, alisema kutokana na utekelezaji wa mipango na mikakati mbalimbali ya kuboresha mazingira ya uwekezaji, mafanikio kadhaa yamepatikana katika kipindi chote cha utekelezaji toka ilipotungwa.

Alitaja baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa uwekezaji wa ndani na ule wa kutoka nje mwaka hadi mwaka.

"Kwa mujibu wa tathmini, takwimu zinaonyesha kiwango cha uwekezaji kutoka nje kimeongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.3 mwaka 1999 hadi Dola za Marekani bilioni 21.2 mwaka 2017. Vile vile, uwiano wa uwekezaji kwa Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 14.7 mwaka 1997 hadi kufikia asilimia 44 mwaka 2018," alifafanua.

# Mgombea aahidi kuboresha stakabadhi ghalani

**Na Thobias Mwanakatwe**

MGOMBEA ubunge Jimbo la Kyela kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Alinanuswe Mwalwage, amesema kama wananchi watampa ridhaa ataangalia namna ya kuboresha mfumo wa stakabadhi gharani, ili uwe na manufaa badala ya kuwa kero kwa wakulima.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wananchi wa kata ya Ngana katika mfululizo wa kampeni zake jimboni humo.

Mwalwage alisema mfumo wa stakabadhi ghalani umekuwa kero katika baadhi ya maeneo kutokana na wakulima kukopwa mazao, hivyo kuwafanya waendelee kukabiliwa na hali ngumu ya maisha.

Mgombea huyo alitoa mfano wa wakulima wa korosho katika Wilaya ya Kyela ambao wamekopwa tangu Oktoba, mwaka jana, na hadi sasa bado hawajalipwa fedha zao.

Alisema akichaguliwa suala la kutafuta soko la uhakika kwa mazao atalipatia ufumbuzi ili wakulima wanufaike na kilimo hicho na hatimaye kuondokana na umaskini.

Aidha, wananchi wa kata hiyo walimwomba kuwasaidia katika ujenzi wa kituo cha afya ambacho walianza kwa kuchangia Sh. milioni 1.3.

Walisema ujenzi wa kituo hicho ulishakwama kutokana na kutopewa ushirikiano na Mwalwage aliahidi kulipatia ufumbuzi suala hilo kwa kuishinikiza serikali itowe fedha za kuanza ujenzi wa kituo.



Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Chalinze mkoani Pwani, Aufemia Ngweta (kushoto), akimshukuru Meneja wa Benki ya NBC tawi la Samora jijini Dar es Salaam, Zubeider Haroun, wakati wa kukabidhi msaada wa mifuko ya saruji iliyotolewa na Benki ya hiyo kwa kushirikiana na Umoja wa Wanafunzi wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya vyoo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum shuleni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi wenye mahitaji watakiwa kujituma kusoma

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI wenye mahitaji maalum katika Shule ya Msingi ya Chalinze mkoani Pwani wamehimizwa kusoma kwa juhudi ili kutengeneza maisha yao ya baadaye, huku wakipewa changamoto ya kujitahidi kila wakati kuwa bora katika masomo na kwa kila kitu wanachofanya.

Hamasa hiyo imetolewa na Meneja wa Benki ya NBC Tawi la Samora jijini Dar es Salaam, Zubeider Haroun, wakati akikabidhi mifuko 75 ya saruji kwa shule hiyo ikiwa ni hatua ya benki kuboresha miundombinu shuleni hapo hususani kwa kujenga choo cha wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Zubeider aliwasihi wanafunzi hao kuwa elimu inaweza kuwapeleka mbali na kutimiza ndoto zao, kwa hivyo wanahitaji kusoma kwa juhudi katika masomo yao huku akiwasisitiza kutokata tamaa hasa wanapopata changamoto katika safari zao za masomo.

"Kwa hivyo nawasihi muweke juhudi katika masomo yenu kwa ajili ya faida ya maisha yenu ya baadaye kwa kuwa elimu ni ufunguo, ambao unafungua milango ya maisha yote," alisisitiza.

Aliongeza kuwa benki hiyo itaendelea kusaidia maendeleo ya elimu ikiwamo kwa wale walio na mahitaji maalum ili kuboresha mfumo wa elimu jumuishi nchini.

"Tumejitolea kusaidia ujenzi wa hitaji hili muhimu la miundombinu ya katika shule hii ili kuboresha upatikanaji wa elimu hususani kwa wanafunzi wenye uhitaji maalum," alisema.

Pia, Zubeider alitoa wito kwa taasisi zingine na watu binafsi kuchangia kwa shule na vituo vya elimu kama nguzo muhimu kuelekea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Akipokea msaada huo Aufemia Ngweta, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa shule hiyo, aliishukuru Benki ya NBC kwa msaada huo na utashi wake katika kusaidia ukuaji wa elimu katika wilaya hiyo. Pia alitoa wito kwa wadau zaidi kusaidia shule hiyo.

"Hapa shuleni kuna watoto wenye ulemavu tofauti, kuna wale walio na ugonjwa wa kupooza kwa ubongo ambao wanahitaji vifaa vingi vya kuchangamsha akili zao, ili waweze kujifunza vitu mbalimbali kama ufundi na ujuzi mwingine kwa maendeleo yao ya baadaye. Kwa hivyo juhudi

# NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL –NEMC

# LIST OF ENVIRONMENTAL EXPERTS CERTIFIED AND REGISTERED BY THE COUNCIL IN THE YEAR 2020

Published pursuant to the Provisions of Regulation 31 of the Environmental (Registration of Environmental Experts) Regulations, 2005 (GN No. 348/2005))

WHEREAS Regulation 31 of the Environmental (Registration of Environmental Experts) Regulations, 2005 directs the Registrar of Environmental Experts to publish each year in the Gazette and the media the list of names of person and firms certified and registered as environmental experts, NOW THEREFORE, the Registrar of Environmental Experts do hereby publish the notice to the general public a list of individual persons and firms of experts dully certified and registered by the National Environment Management Council as Environmental Experts who are entitled to undertake Environmental Impact Assessment (EIA) and Environmental Audit (EA) of development projects in Tanzania mainland.

## I. INDIVIDUAL PERSONS CERTIFIED AND REGISTERED AS ENVIRONMENTAL EXPERTS TO UNDERTAKE ENVIRONMENTAL IMPACT ASSESSMENT (EIA)

| S/N | FULL NAME OF APPLICANT | SPECIALIZATION | POSTAL ADDRESS | TEL. NO | EMAIL ADDRESS |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | ELIANA GODLUCKSON KAWICHE | BSc. in Environmental Engineering | P.O.BOX 1964, DAR ES SALAAM | +255 685 639 219 | elianakawiche@gmail.com |
| 2 | ABDUL-LATIF HABIB MOHAMMED | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 42726, DAR ES SALAAM | +255679 423 272 | abdhamod07@gmail.com |
| 3 | EMMANUEL MMASI KITEMA | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 42726, DAR ES SALAAM | +255 753 998 816 | mmasi114@gmail.com |
| 4 | SILVIA AUTOPHACE KALLETA | BSc. in Environmental Studies | P.O.BOX 133, MWANZA | +255 762 250 902 | sylviautophace@gmail.com |
| 5 | SEFU ALLY SEFU | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 79135, DAR ES SALAAM. | +255 717 633 013 | sefusefu995@gmail.com |
| 6 | MUGADI GOLEHA | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 3036, MWANZA. | +255 764 957 716 | yemugagoleha@gmail.com |
| 7 | PETER MUNIKO THOMAS | BSc. in Electronics Science and Communication | P.O.BOX 5191, DAR ES SALAAM. | +255 767 410 050 | petermuniko68@yahoo.com |
| 8 | GRACE CHRISTIAN MARANDU | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 79844, DAR ES SALAAM. | +255 765 948 789 | gracetaji@gmail.com |
| 9 | TEDDY GERALD KANJONGO | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 3519, DAR ES SALAAM. | +255 755 844 080 | kanjongoteddy@gmail.com |
| 10 | RHODA NYAMWIZA MUTALEMWA | MSc. in Engineering<br>BSc. in Environmental Laboratory Science and Technology | P.O.BOX 71829, DAR ES SALAAM | +255 655 624 385 | rmutalemwa@gmail.com |
| 11 | DR. CLARA KWEKA MSALE | PhD. in Planning and Governance<br>MSc. in Urban Planning and Management<br>BSc. in Urban and Regional Planning | P.O.BOX 35774, DAR ES SALAAM | +255 652 777 512 | nicasclara@yahoo.com |
| 12 | AMINIEL B. MLUNGWANA | BSc. in Environmental Laboratory Science and Technology | P.O.BOX 45834, DAR ES SALAAM | +255 659 713 027 | mlungwanaamy@gmail.com |
| 13 | NELLY SETH MWAKATUNDU | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 23266, DAR ES SALAAM. | +255 714 774 909 | neleseti@gmail.com |
| 14 | MWANAHAMISI M. HASHIM | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 35892, DAR ES SALAAM. | +255 654 561 532/+255 765 401 | mishyhashy@gmail.com |
| 15 | RICHARD PETER MLUNDE | BSc. in Environmental Engineering | P.O.BOX 60444, DAR ES SALAAM. | +255 657 038 633 | richardmlunde13@gmail.com |
| 16 | ANNA APOLINARY MALLYA | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 427226, DAR ES SALAAM | +255 766 473 939 | siaapolo@gmail.com |
| 17 | PENDO Z. NASSARY | BSc. in Environmental Engineering | P.O.BOX 33516, DAR ES SALAAM | 255 718 392 406 | nassarypendo@gmail.com |
| 18 | JOHN PETER KACHEMA | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 100182, DAR ES SALAAM. | +255 768 758 768/+255 719 777 | peterjohn558@yahoo.com |
| 19 | AMANI SHABANI KYANGO | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 1857, DODOMA, | 0712-732171 | shabaniamani@gmail.com |
| 20 | PAGU JULIUS | MSc. in Fisheries and Aquaculture<br>BSc. in Fisheries and Aquaculture | Marine Park and Reserve Unit<br>P.O.BOX 7565, DAR ES SALAAM | 0786-604434 | juliuspagu@gmail.com |
| 21 | DR. INNOCENT JOSEPH ENOS ZILIHONA | PhD. Environmental Management<br>MSc. in Environmental Biology<br>BSc. in Forestry | Institute of Rural Development Planning<br>P.O Box 138, DODOMA | 0627989710 | Innocent.zilihona@irdp.ac.tz |
| 22 | ROBERT R DAUDI | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 2031MAGU-MWANZA | 0656-267003 | Robertdaudi@gmail.com |
| 23 | EMMANUEL S. MOGENGE | BA. in Environmental Disaster | P.O. BOX 6048 MWANZA | 0622-626365 | Emogenges58@gmail.com |

215913902

# TANGAZO

| S/N | FULL NAME OF APPLICANT | SPECIALIZATION | POSTAL ADDRESS | TEL. NO | EMAIL ADDRESS |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Management | | | |
| 24 | WILSON FRANK MAANGA | MSc. in Climate Change<br>BSc. in Wildlife Management | P.O. BOX 3134 ARUSHA | 0785-856200 & 27 29700404 | Wilson.maanga@tanzaniaparks.go.tz |
| 25 | CLEMENTINA JOSEPH SIMPLISI | MA. in Environmental Planning and Management<br>BA. in Environmental Planning and Management | P.O.BOX 1249, DODOMA | +255 656 396 226 | clementinasimplisi@gmail.com |
| 26 | EDITH WILLIAM MAKUNGU | BSc. with Geology | P.O.BOX 63154, DAR ES SALAAM | 0754 928486 | dithmakungu@gmail.com |
| 27 | ENG. BENJAMIN J. MCHWAMPAKA | MSc. in Environmental Studies<br>BSc. in Mining Engineering | P.O.BOX 63154 DAR ES SALAAM | +255 754 366 968 | mchwampakajoel@gmail.com |
| 28 | BEATRICE SIMON MOSHI | MA. in Natural Resources Management<br>BSs. in Wildlife Management | P.O.BOX 2637, DODOMA | +255 752 229 904/+255 672 796 298 | simonbeatrice85@yahoo.com |
| 29 | KELVIN ARTHUR. MANG'ENYA | BSc in Environmental Science and Management | P.O.BOX 1699, ARUSHA. | +255 716 117 458 | arthur92.ka@gmail.com |
| 30 | LUCY JACOB SALLA | BA in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 12145, DAR ES SALAAM | +255 742 434 875 | sallalucy19@gmail.com |
| 31 | FREDY LISTER MARO | MA in Development studies & MSc Environmental science management | P.O.BOX 395, DODOMA. | +255 713 803084 | fredymaro@yahoo.com |
| 32 | GILBERT GRID KIBANDA | BSc in Environmental Laboratory Science and Technology | P.O.BOX 22125 DAR ES SALAAM. | +255 679 972 280/ +255 622 873 412 | gridkibanda@gmail.com |
| 33 | HAPPINESS M. SOSPETER | BSc in Chemistry | P.O.BOX 31285, DAR ES SALAAM. | +255 752 851 738 | happinessdiana@gmail.com |
| 34 | PETER VICTOR MGENI | BSc in Environmental Engineering | P.O.BOX 34240, DAR ES SALAAM. | +255 783 993 138 | petermgeni@gmail.com |
| 35 | KIVUMA SAIDI | BSc in Municipal and Industrial Services Engineering | P.O.BOX 80977, DAR ES SALAAM. | +255 653 924 118 | kivumasaidi5@gmail.com |
| 36 | AKONDA EDSON MWANGUNGA | BSc Environmental Science and Management | P.O.BOX 11364, DAR ES SALAAM. | +255 753 287 799 | amwangunga@yahoo.com |
| 37 | SARA MALLE | BSc in Environmental Science and Management | P.O.BOX 6048, DAR ES SALAAM. | +255 757 970 052 | saramalle82@gmail.com |
| 38 | MAXMILIAN MAHANGILA | BSc in Land Management and | P.O.BOX 18000, DAR ES | +255 713 437 415 | mahangila@yahoo.com |
| 39 | LINUS W. MATERU | MSc Engineering Water and Waste Engineering | P.O.BOX 5592, DAR ES SALAAM. | +255 713 337 991 | linusmateru@yahoo.com |
| 40 | SOSPETER JOSEPH ISAYA | BSc in Environmental Engineering | P.O.BOX 1683, DAR ES SALAAM. | +255 783 931 501 | sospeterjay@gmail.com |
| 41 | BARNABAS FERDINAND JACHI | MSc. Community Economic Development | P.O.BOX 62584, DAR ES SALAAM | +255 754 491 347 | barnabasjachi@gmail.com |
| 42 | ROY BROWN NAMGERA | BSc with Geology and Master of Economic Geology | P.O.BOX 33516, DAR ES SALAAM. | +255 717 251 000 | roynamgera@gmail.com |
| 43 | MARTHA M. NIKODEMUS | BSc in Environmental Science and Management | P.O.BOX 5035, DAR ES SALAAM | +255 743 287 465/+255 672 233 078 | marthammassy@gmail.com |
| 44 | WENCESLAUS SYLVESTER MUTYAMA | MA in Natural Resources Assessment and Management | P.O.BOX 35091, DAR ES SALAAM. | +255 784 709 732 | mutyamasw2016@gmail.com |
| 45 | ESTHER PRAYGOD | BA in Environmental Planning and Management | P.O.BOX 25333, DODOMA. | +255 767 413 628 | estherpraygod@gmail.com |
| 46 | GERALD XEERANG'W GISIPUT | BA in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 15070 ARUSHA | 0758-986543 | geraaldshirra@gmail.com |
| 47 | JACKLINE JACOB RINGO | MA in Environmental Planning and Management | P.O. BOX 138, DODOMA | 0755-045080 | ringojackline@gmail.com |
| 48 | LADISLAUS SWEETBERTH MAGENI | BA Environmental Planning and Management | P.O. BOX 41,NZEGA | 0769 – 731540 | ladimageni@gmail.com |
| 49 | JACKSON C. NGOWI | MSc in Environmental Studies | P.O. BOX 2324 KILOLO, IRINGA | 0654290091 | jacksngowi@gmail.com |
| 50 | SOSPETER GODBLESS MAYA | BA Environmental Planning and Management and MA in Environmental Planning and Management | P.O. BOX 233 DODOMA | 0767-320476 | sospetermaya@gmail.com |
| 51 | MAJAHA MALONGO | BSc in Environmental Planning and Management | P.O. BOX 138 DODOMA | 0769-446786 | majahamalongo@gmail.com |
| 52 | FAITH COSPETIN MOSHI | BA in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 1249 DODOMA | 0762270874 | Faithmoshi25@gmail.com |
| 53 | IRENE RICHARD KYANDO | BSc in Environmental Science and Management | P.O. BOX 305, MPWAPWA DODOMA | 0762-956161 | Irene90kyando@gmail.com |
| 54 | SENGATI KADILANHA | MSc in Natural Resources Assessment and Management &<br>BSc in Chemistry Minor in Botany and Zoology | P.O. BOX 943, BUTIAMA MARA | 0787-577038 | sengatik@yahoo.com |
| 55 | JANETH FAHAMUEL NKURWA | BA in Geography and Environmental Studies | P. O.BOX 13585, DAR ES SALAAM. | +255 765 126 627/+255 719 480 554 | janethnkurwa@gmail.com |
| 56 | JOYCE ABRAHAM KASEBELE | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 18000 DAR ES SALAAM. | +255 716 647 675 | jkasebele@gmail.com |
| 57 | NYANDARO MTEKI | PhD in Environmental and Social Studies | P.O.BOX 35670 DAR ES SALAAM | +81-3-5276-3930 | a9079@n-koei.co.jp /nyandaromteki@gmail.com |
| 58 | KELVIN THOMAS | BSc in Bio Processing & Post Harvesting Engineering | P.O.BOX 6840, MWANZA | +255 763 985 119 | kelvintoma2015@gmail.com |
| 59 | LINDA MELKIOR | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 9670, DAR ES SALAAM | +255 755 208 142 | lindakavishe@gmail.com |
| 60 | DEODATHA FIDELIS AGRICOLA | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 99229, DAR ES SALAAM. | +255 783 253 848/+255 767 933 449 | deodath1990@gmail.com |
| 61 | GODLISTEN MOSSES MBISE | BA in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 842 ARUSHA | 0766-735420 | Godlistenmbise120@gmail.com |
| 62 | UPENDO ELIAKUNDA KIMARO | BA in Geography and Environmental Studies | C/O DR. AMOS JAMES IBRAHIM<br>INSTITUTE OF TAX ADMINISTRATION<br>P.O.BOX 9321 DAR ES SALAAM | 0758-209287 | Upendokimaro8@gmail.com |

## TANGAZO

**II. INDIVIDUAL PERSONS CERTIFIED AND REGISTERED AS ENVIRONMENTAL EXPERTS TO UNDERTAKE ENVIRONMENTAL AUDIT (EA)**

| S/N | FULL NAME OF APPLICANT | SPECIALIZATION | POSTAL ADDRESS | TEL. NO | EMAIL ADDRESS |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BENEDICTOR LUCAS | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 1699 ARUSHA. | +255 743 091 863 | benylucas7@gmail.com |
| 2 | DANIEL J. MAGANGA | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 15070, ARUSHA. | +255 767 500 059 | magangadaniel174@gmail.com |
| 3 | MOSSES NG'HOMANGO | BSc. in Electrical Engineering | P.O.BOX 35670, DAR ES SALAAM | +255 767 869 969 | mngomango@yahoo.com |
| 4 | KELVIN THOMAS | BSc. in Bio Processing and Post Harvest Engineering | P.O.BOX 6840, MWANZA. | +255 763 985 119 | kelvintoma2015@gmail.com |
| 5 | KAMARIYA MIKIDADI MOHAMED | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 36086, DAR ES SALAAM. | +255 653 577 247 | qamariyamohamed@gmail.com |
| 6 | DR. CLARA KWEKA MSALE | PhD. in Planning and Governance;<br>MSc. in Urban Planning and Management and<br>BSc. in Urban and Regional Planning | P.O.BOX 35774, DAR ES SALAAM. | +255 652 777 512 | nicasclara@yahoo.com |
| 7 | EVERLYN ESTOMIAH SWAI | MSc. in Environment and Natural Resource Economics<br>BSc. in Wildlife Management | P.O.BOX 7740, MWANZA. | +255 714 185 758 | eveesto11@gmail.com |
| 8 | DEOGRATIUS S. LYIMO | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 2435, MBEYA. | +255 657 497 929 | lyimo4deogratius@gmail.com |
| 9 | INNOCENT GURANYWA | BSc. in Environmental Engineering | P.O.BOX 12519, DAR ES SALAAM | +255 759 547 070 | iguranywa@yahoo.com |
| 10 | RENATUS JOSEPH | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 42726, DAR ES SALAAM. | +255 764 090718 | godyfghati@gmail.com |
| 11 | JAMES AMANI NGAKONDA | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 491565, DAR ES SALAAM. | +255 766 491 565 | ngakonda95@hotmail.com |
| 12 | PENDO Z. NASSARY | BSc. in Environmental Engineering | P.O.BOX 33516, DAR ES SALAAM. | +255 718 392 406 | nassarypendo@gmail.com |
| 13 | THOBIAS SONDA MATHEW | MSc. in Environmental Studies<br>BSc. Education Majoring in Physics and Chemistry | P.O. BOX 11774 DAR ES SALAAM | 0763-732967 | thobiassonda@yahoo.com |
| 14 | REUBEN M. MAKALLA | BA. in Environmental Disaster Management | Air Port Road<br>Plot no 8, Block F, Opp Rock city Mall,<br>P.O. BOX 526, MWANZA | 0715-906699 | makallarm@gmail.com & remacotanzania@gmail.com |
| 15 | CHRISTOPHER NGWANYEMI MDOE | MA. in Environmental Planning and Management<br>BA. in Environmental Planning and Management | Institute of Rural Development Planning<br>P.O. BOX 11957<br>MWANZA- TANZANIA | 0715-124320 | christmdoe@gmail.com |
| 16 | ROBERT R. DAUDI | BSc. in Environmental Science and Management | P.O. BOX 2031 MAGU-MWANZA | 0656-267003 | Robertdaudi@gmail.com |
| 17 | MARCO MCHOME | MSc. in Environmental Impact Assessment<br>BA. in Geography and Environmental Studies | Kimara Temboni, Temboni B Street, Shina No 02<br>P.O.Box 13033 DAR ES SALAAM | 0787-695219 | mchomem@yahoo.com |
| 18 | CHRISTINA REUBEN BUSENGHWA | BSc. in Environmental Science and Management | P.O. BOX 124, MWANZA | 0689-067867 | Reuchristina1@yahoo.com |
| 19 | GODFREY NARTUS MWITA | BSc. in Forestry | P.O.BOX 2006 IRINGA | 0784-894256 | godmwita@gmail.com |
| 20 | SOSPETER GODBLESS MAYA | BA. in Environmental Planning and Management<br>MA. in Environmental Planning and Management | P.O. BOX 233 DODOMA | 0767-320476 | sospetermaya@gmail.com |
| 21 | HAMZA RAJABU | BSc. in Municipal and Industrial Services Engineering | P.O.BOX 72765, DAR ES SALAAM | +255 713 788 282 | hamzarajabu36@gmail.com |
| 22 | EMMANUEL STEPHEN BUNDALA | BA. in Geography and Environmental Studies | P.O.BOX 72834, DAR ES SALAAM. | +255 785 915 599 | bundama14@gmail.com |
| 23 | ELIUDI GRANTON MWAMBOPE | BSc. in Municipal and Industrial Services Engineering | P.O.BOX 4604, MBEYA. | +255 759 612 743/+255 676 612 743 | mwambopeeliudi85@gmail.com |
| 24 | ROY BROWN NAMGERA | MSc Economic Geology & MSc. in Natural Resource Assessment & Management | P.O.BOX 33516, DAR ES SALAAM. | +255 717 251 000 | roynamgera@gmail.com |
| 25 | WENCESLAUS SYLVESTER MUTYAMA | MA in Natural Resources Assessment and Management | P.O.BOX 35091, DAR ES SALAAM. | +255 784 709 732 | mutyamasw2016@gmail.com |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 26 | CANUTE BENEDICT HYANDYE | BSc. in Environmental Science and Management & MSc of Engineering in Environmental Science | Institute of Rural Development Planning P.O Box 138, DODOMA | 0769-777715 | chyandye@irdp.ac.tz |
| 27 | JUMA HUSSEIN KILONGO | BSc. in Environmental Science and Management | P.O. BOX 16221 DAR ES SALAAM. | 0652060010 | kilongojj@gmail.com |
| 28 | EDITH WILLIAM MAKUNGU | BSc. with Geology | P.O. Box 63154 DAR ES SALAAM | 0754 928486 | dithmakungu@gmail.com |
| 29 | SENGATI KADILANHA | MSc. in Natural Resource Assessment & Management | P.O. BOX 943, BUTIAMA MARA | 0787-577038 | sengatik@yahoo.com |
| 30 | ENG. BENJAMIN J. MCHWAMPAKA | MSc. in Environmental Studies BSc. in Mining Engineering | P.O. Box 63154 DAR ES SALAAM | 0754-366968 | mchwampakajoel@gmail.com |
| 31 | MWANAHAMISI M. HASHIM | BSc. in Environmental Science and Management | P.O.BOX 35892, DAR ES SALAAM. | +255 654 561 532/+255 765 401 634 | mishyhashy@gmail.com |
| 32 | NEEMA KIJAZI | BSc. in Environmental Engineering | P.O.BOX 35176, DAR ES SALAAM | +255 746 606 006 | kijazineema@yahoo.com |

### III. LIST OF FIRMS THAT ARE CERTIFIED AND REGISTERED TO UNDERTAKE ENVIRONMENTAL IMPACT ASSESSMENT (EIA)

| S/N | FULL NAME OF FIRM | POSTAL ADDRESS | TEL NO. | EMAIL ADDRESS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ECONAT Consultants Limited | P.O.BOX 35892, DAR ES SALAAM. | +255 739359 044 | econatconsultant@gmail.com |
| 2 | SIMCHO Consulting (T) LTD | KIMARA TEMBONI P.O. BOX 13033 DAR ES SALAAM | 0754-271175 | simchoconsulting@gmail.com |
| 3 | ENVIRICH Consultant Limited | P.O.BOX 2786, DAR ES SALAAM | +255 715 767 144 | Richard.mgambwa@gmail.com |
| 4 | Alpha Business Management Company Limited | P.O.BOX 15284, DAR ES SALAAM. | +255 712 523 315 | bernadetha@alphabm.com |
| 5 | RSK Environment (East Africa) Ltd | P.O.BOX 3519, DAR ES SALAAM. | +255 744 212 981 | nmwesigwa@rsk.co.uk www.rskgroup.com |
| 6 | CRM Land Consult (T) Limited | P.O.BOX 35774, DAR ES SALAAM. | +255 747 844 246 | crmlandconsult@gmail.com |
| 7 | JAVALI Company Limited | P.O.BOX 35176, DAR ES SALAAM. | +255 767 359 044/+255 655 359044 | javali.limited@gmail.com |
| 8 | WESH Consulting Limited | P.O.BOX 35478, DAR ES SALAAM. | +255 752 575 989 | weshconsultingltd@gmail.com |
| 9 | SIGNMARK Africa Co Limited | P.O. BOX 71341 Dar es Salaam | 0719-604140 | signmarkafrica@gmail.com |
| 10 | KASUMO Technologies Limited | P.O.BOX 77228, DAR ES SALAAM. | +255 22 2667333 / 0718 769114 | info@kasumo.co.tz |
| 11 | Shwekelela's Company Limited | P.O.BOX 384, GEITA. | +255 755 637 931 | shwekelelap@yahoo.com |

### IV. LIST OF FIRMS THAT ARE CERTIFIED AND REGISTERED TO UNDERTAKE ENVIRONMENTAL AUDIT (EA)

| S/N | FULL NAME OF FIRM | POSTAL ADDRESS | TEL NO. | EMAIL ADDRESS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ECONAT Consultants Limited | P.O.BOX 35892, DAR ES SALAAM. | +255 739359 044 | econatconsultant@gmail.com |
| 2 | ENVIROWISE | P.O.BOX 8747, DAR ES SALAAM. | +255 657 088 887 | info@envirowise.co.tz lilian@envirowise.co.tz |
| 3 | ENVIRICH Consultant Limited | P.O.BOX 2786, DAR ES SALAAM. | +255 715 767 144 | Richard.mgambwa@gmail.com |
| 4 | RSK Environment (East Africa) Ltd | P.O.BOX 3519, DAR ES SALAAM. | +255 744 212 981 | nmwesigwa@rsk.co.uk |
| | | | | www.rskgroup.com |
| 5 | Shwekelela's Company Limited | P.O.BOX 384, GEITA. | +255 755 637 931 | shwekelelap@yahoo.com |

The public is reminded that no person or firm shall conduct an Environmental Impact Assessment (EIA) or Environmental Audit (EA) or carry any activity relating to the conduct of an Environmental Impact Study or Environmental Audit as provided for under the Environmental Management Act CAP 191, unless that person or firm is dully certified and registered in accordance with the Environmental (Registration of Environmental Experts) Regulations, 2005.

It should also be noted that, foreign environmental experts or firm of experts may be certified by the Council to prepare **SPECIFIC** Environmental Impact Assessment or Environmental Audit studies if such an expert or firm meets the conditions stipulated in the Environmental (Registration of Environmental Experts) Regulations, 2005. **(GN. No.348/2005)**

**For further information please contact;**
**Dr. Menan Jangu**
**Registrar of Environmental Experts,**
**National Environment Management Council - NEMC.**
**P.O.BOX 63154, DAR ES SALAAM.**
**Date: 28th August, 2020**



# Ujerumani kusaidia elimu kwa watoto

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

SERIKALI ya Ujerumani imeihakikishia Tanzania kuwa itaendelea kushirikiana nayo katika kuhakikisha watoto wa kitanzania wanapata elimu bora.

Mkuu wa Kitengo cha Ushirikiano wa Maendeleo katika Ubalozi wa Ujerumani nchini, Dk. Katrin Bornemann, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha pamoja kati ya wawakilishi kutoka ubalozi wa Ujerumani na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kilichofanyika jijini hapa.

Alisema nchi hiyo imekuwa na ushirikiano na Tanzania kwa muda mrefu kwenye masuala ya sekta ya elimu, hivyo itaendeleza ushirikiano huo ili watoto hao wapate elimu bora.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, alisema katika kikao hicho nchi hizo zimekubaliana kuendeleza mashirikiano kwenye elimu ya juu, ufundi na msingi ili kuhakikisha watoto wa kitanzania wanapata ujuzi na kushiriki katika ujenzi wa Taifa.

Alibainisha kuwa kwa sasa nchi inatekeleza miradi mikubwa ya ujenzi hivyo kuna uhitaji wa wataalamu wenye ujuzi katika eneo.

"Tunajenga reli ya kisasa ya umeme SGR, madaraja na ipo miradi mingine mikubwa inatekelezwa, pamoja na kwamba tunao wataalamu wetu nchini bado tunahitaji wajiendeleze ili kupata ujuzi zaidi. Kwa hiyo tumezungumza nao kuona ni namna gani tunaweza kushirikiana kuwezesha mafunzo kwa vijana hapa nchini na hata nchini kwao," alisema Dk. Akwilapo.

Akizungumzia uimarishaji wa elimu ya msingi, Katibu Mkuu huyo alisema pia wamekubaliana kushirikiana kuongeza ujuzi wa walimu katika mbinu mpya za ufundishaji ikiwa ni pamoja na kutoa vifaa vya kufundishia.

Ujerumani kupitia Shirika lake linalojihusisha na mabadilishano ya wanafunzi (DAAD) imekuwa ikitoa ufadhili wa masomo kwa wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.




Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Kati, Chabu Mishwaro (kulia), akikabidhi mfano wa funguo ya trekta kwa mkulima Stanley Nyakunga kutoka Kibaigwa wilayani Kongwa, ukiwa ni mkopo kutoka kampuni ya ETC Agro Tractors and Implements Ltd lenye thamani ya Sh. milioni 42, jijini Dodoma juzi. Mikopo hiyo kwa wakulima imedhaminiwa na benki hiyo. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Wakulima 100 wakopeshwa matrekta

**Na Ibrahim Joseph**,
DODOMA

WAKULIMA 100 nchini wamepata mkopo wa matrekta kwa ajili ya kuinua kilimo cha biashara kwa udhamini wa Benki ya CRDB.

Akizungumza jana wakati akikabidhi trekta kwa mkulima kutoka Wilaya ya Kongwa, Meneja Masoko wa Kampuni ya kuuza matrekta ya Etc Agro Tractors and Implements Ltd, Justine Andrew, alisema kutokana na wakulima kuhitaji zana hizo za kilimo ili kupanua shughuli zao, benki hiyo imewadhamini kupata matrekta hayo.

Alisema kampuni hiyo imeingia mkataba na benki hiyo wa kuwakopesha wakulima wadogo, kati na wakubwa kwa masharti hayo bila ubaguzi. Alitaja mikoa ambayo wakulima wamenufaika na zana hizo kuwa ni Mbeya, Morogoro, Dodoma, Kagera, Iringa, Manyara na Simiyu.

"Matrekta yanayouzwa na kampuni yetu ni kuanzia Sh. milioni 24 hadi Sh. milioni 80 kulingana na ukubwa wa trekta analohitaji mkulima," alisema. Naye mkulima kutoka Kibaigwa, Stanley Nyakunga, alisema wakulima wamekuwa wakisahaulika kupata mikopo kutokana na kukosa udhamini.

"Wakulima hawaogopi mikopo ila wanachoshindikana na taasisi za kifedha ni masharti pale inapotokea hali ya msimu wa kilimo unakaa vibaya kwa kukosa mavuno kwa sababu ya mvua ndogo," alisema.

Aliongeza: "Uzuri sisi wakulima mali zetu zinafahamika na hali ya kilimo haijifichi kama kuna mvua nzuri hali ya mazao inaonekana, lakini ikitokea hali mbaya ya mavuno inaonekana haifichiki."

Alisema hali ya kilimo ikiwa sawa hakuna mkulima anayependa kuingia kwenye matatizo na taasisi hizo za kifedha isipokuwa kinachotakiwa ni kufanya kazi kwa karibu, ili kujua hali ya mavuno kwa mwaka husika.

Kwa upande wake, Meneja wa benki ya CRDB Kanda ya Kati, Chabu Miswaro, alisema benki hiyo imepanua wigo wa kuwahudumia wananchi kwa kuingia kuwadhamini wakulima kupata mikopo ya zana za kilimo na matrekta.

Miswaro alitaja masharti ya kupata mikopo hiyo kuwa ni mkulima anatakiwa kuwa na kitambulisho cha Taifa, mpigakura au hati ya kusafiria na awe na umri wa kuanzia miaka 21.

Aliongeza kuwa mkulima huyo haitaji kuwa na dhamana ya ziada kwa sababu trekta lake litatumika kama dhamana ya mkopo huo atakaohitaji kuchukua.

Alisema benki hiyo imeingia mkataba na kampuni tatu za kuuza na kusambaza zana

# Usimamizi mradi watega waganga wa wilaya, mikoa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitasita kumchukulia hatua Mganga Mkuu wa Mkoa au Wilaya atakayebainika kushindwa kusimamia fedha za mradi wa Boresha Macho.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa(Tamisemi), Dk. Ntuli Kapologwe, alitoa kauli hiyo jana kwenye uzinduzi wa mradi wa Boresha Macho unaotekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la Sightsavers kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Uingereza (UKAID).

Dk. Kapologwe alisema mradi huo unagharimu Sh. bilioni sita lazima kuwapo na usimamizi wa fedha mkubwa wa fedha hizo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mkurugenzi huyo alisema kama kuna mganga mkuu ambaye atashindwa kusimamia vizuri fedha za mradi huo atajieleza kwanini hawezi kusimamia.

"Tuchukue mradi kama mtoto wetu na malengo tuliyoweka lazima yafanikiwe, hatutamvumilia mtu yeyote aidha anatoka shirika lisilo la kiserikali au serikalini ambaye hatatekeleza inavyotakiwa, kwansababu hizi fedha zimeletwa kwa ajili ya Watanzania na wanapaswa kunufaika na kila uwekezaji unaofanywa kwenye macho," alisema.

Alieleza kuwa suala la ubora wa kazi itakayofanyika ni la msingi ili mradi ufanyike kwa malengo yaliyokusudiwa, huku akisema pale itakapobainika mradi hautekelezwi ipasavyo serikali haitasita kuchukua hatua.

"Kila senti moja ambayo imetolewa kwa ajili ya mradi huu lazima iwafikie walengwa ambao ni wananchi, sisi TAMISEMI na Wizara ya Afya tutafanya ufuatiliaji wa karibu ili kuona kama kuna thamani ya fedha kwenye utekelezaji wa mradi huu, Sh. bilioni sita za mradi tunataka tuone vitu," alisema.

Alisema serikali imekuwa ikiendelea kuimarisha huduma za afya kwa wananchi ambapo zimeshuka hadi ngazi za vituo vya afya.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Wizara ya Afya anayeshughulia magonjwa yasiyoambukiza, Dk. James Kiologwe, alisema asilimia moja ya Watanzania wanakabiliwa na tatizo la uoni ambao unasababisha kupata upofu.

Hata hivyo, alisema asilimia 75 ya matatizo yanayosababisha upofu yanazuilika na wizara inajivunia kufanya kazi na wadau kuhakikisha idadi hiyo ya watu wanapata tiba ili wasipate upofu.

"Katika ushirikiano huo kuna mambo tunajivunia hadi sasa, tumeweza kuratibu vizuri wadau, tunajua katika viwango vya kimataifa tunatakiwa kuwa na hospitali moja ya kutoa huduma za upasuaji kwa watoto wanaopata matatizo ya macho, tunafurahi hadi sasa kuna hospitali nne ambazo zinauwezo huo," alisema.

Awali, Ofisa Miradi, Tathmini na Ufuatiliaji kutoka shirika hilo, Neema Kalole, alisema mradi huo utagharimu kiasi cha Sh. bilioni sita na unatarajiwa kupima na kutoa huduma za macho kwa watu 150,000 huku kati yao 13,500 watakaobainika na mtoto wa jicho watafanyiwa upasuaji.

Aidha, alisema mradi huo pia utaongeza uelewa kwa watu 650,000 kuhusu umuhimu wa kupata huduma za macho.

"Mradi utafikia halmashauri tano kati ya tisa za Mkoa wa Morogoro na kwa Mkoa wa Singida halmashauri zote tisa zitanufaika," alisema.





# Wachimbaji waeleza sababu kukopa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WACHIMBAJI wadogo wa madini mkoani hapa, wamesema wanalazimika kukopa fedha kwa watu binafsi na taasisi zisizokuwa rasmi kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli zao kutokana na kukataliwa na taasisi rasmi kwa madai kuwa hawana vigezo vya kukopesheka.

Waliyasema hayo juzi jijini hapa wakati wa uzinduzi wa mafunzo ya mikopo ya vitendea kazi vya kuchimbia madini kwa wachimbaji wadogo, wa kati na wakubwa kutoka katika mikoa ya Mbeya na Songwe yaliyoandaliwa na benki ya NMB.

Mmoja wa wachimbaji hao, Aidan Msigwa, mchimbaji mdogo wa dhahabu katika Wilaya ya Chunya, alisema pamoja na wakopeshaji binafsi riba yao ni kubwa, lakini hawana masharti magumu kama benki.

Alisema yeye ni mmoja wa watu walioumizwa na mikopo ya wakopeshaji binafsi kwa madai kuwa alienda kuomba mkopo kwenye moja ya benki ambayo ilimnyima na hivyo kuamua kwenda kukopa kwa mtu binafsi. Alisema alikopeshwa Sh. milioni 50 na akawa anatakiwa kulipa Sh. milioni 300 ndani ya miezi mitatu, lakini akashindwa na sasa deni lake limepanda na kufikia Sh. milioni 900.

"Hawa wakopeshaji binafsi wanatuumiza na wakati mwingine wanadai kwa vitisho kabisa, unaweza ukawa umelala usiku anakuja kukuamsha, mimi mpaka sasa nimeshalipa zaidi ya nusu ya deni langu na nitamaliza, ila tunawashukuru NMB wamekuja kutuokoa," alisema Msigwa. Mwenyekiti wa wachimbaji wa Mkoa wa Mbeya, Leonard Manyesha, aliishukuru NMB kwa kuanzisha mikopo hiyo kwa wachimbaji kwamba itawasaidia kuongeza tija kwenye sekta ya uchimbaji wa madini.

Alisema kwa muda mrefu wachimbaji wadogo walikuwa wanatumia zana duni za kuchimbia ikiwamo majembe, sululu na zana zingine ndogo, lakini walikuwa wanapata pesa.

Manyesha alisema walikuwa wanashangaa benki zilivyokuwa zinagoma kuwakopesha wakati wamekuwa wakionyesha uaminifu wa kuwalipa wakopeshaji binafsi.

Meneja wa NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Straton Chilongola, alisema lengo la benki hiyo ni kuwafikia wachimbaji wa mikoa mbalimbali nchini ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika na kuinua uchumi wa wachimbaji.

Alisema benki hiyo inatambua kuwa wachimbaji wadogo hawapo kwenye mfumo rasmi wa uchumi, lakini wameandaa mfumo mzuri ambao utasaidia wachimbaji kukopa na kurejesha.

"Tumeandaa utaratibu wa kuwafungulia akaunti wachimbaji wadogo na hii ndiyo itakuwa hatua ya kwanza ya kutambulika na serikali kuwa ni wachimbaji halali, sisi tumeitikia wito wa kulisaidia kundi hili," alisema Chilongola.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema ana orodha ndefu ya watu wanaokopesha fedha kwa wananchi bila kufuata sheria za nchi na akawataka kuacha mara moja shughuli hiyo.

Alisema endapo wakopeshaji hao wataendelea, atayatangaza hadharani majina yao na kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kutaifisha mali zao.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika (kushoto), akikagua mradi wa ufugaji kuku unaomilikiwa na vijana wa Kata ya Ilembo, wilayani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mdau akabidhi UWT vijana 30 aliojitolea kuwasomesha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MDAU wa Maendeleo mkoani Mbeya, Ndele Mwanselela, ameukabidhi uongozi wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) mkoa, vijana 30 ambao amewasomesha bure kwenye shule yake ya Patrick Mission ya jijini Dar es Salaam kuanzia kidato cha kwanza mpaka cha nne.

Mwaselela alikabidhi vijana hao juzi kwenye hafla iliyofanyika katika Shule ya Sekondari ya kutwa ya Mbeya na kuutaka uongozi wa UWT kuendelea kuwalea vijana hao, ili wafikie malengo yao ya maisha.

Alisema, amewasomesha watoto hao bure na aliamua kufanya hivyo kama sehemu ya kutoa sadaka kwa watoto hao ambao wengi ni yatima na wengine wanatoka kwenye familia ambazo hazina uwezo wa kuwasomesha.

Mwaselela alisema bado wapo watoto wengine ambao anaendelea kuwasomesha kwenye shule yake akiwamo mtoto wa marehemu, Agnes Gerald 'Masogange' na kwamba ataendelea kuwasomesha.

"Leo tumekabidhi watoto ambao wamehitimu kidato cha nne, kati ya watoto hawa wote wamefaulu kwa kupata daraja la kwanza isipokuwa wanne ambao wamepata daraja la pili," alisema Mwaselela.

Baadhi ya watoto hao walimshukuru Mwaselela kwa kuwasaidia na kwamba watahakikisha wanasoma na kufika mpaka elimu ya chuo kikuu ili waje walisaidie taifa.

Rebeca Mwaibingila, ambaye ni miongoni mwa wasichana waliofanya vizuri kitaifa kwa kushika nafasi ya saba, alisema elimu aliyoipata itamsaidia kufikia ndoto yake ya kuwa daktari na kwamba asingeweza kuifikia bila kupatiwa msaada huo.

# Samia aahidi mabwawa ya kuvuna maji ya mvua

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA mwenza wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan, amesema endapo chama hicho kitashinda kwenye uchaguzi wa Oktoba 28 mwaka huu, serikali itajenga mabwawa ya kuvunia maji ya mvua katika kila wilaya nchini ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa huduma hiyo.

Aliyasema hayo wakati alipokuwa anazungumza na wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwenye mikutano mbalimbali ya kuomba kura za chama hicho.

Alisema mbali na ujenzi wa mabwawa hayo pia serikali itahakikisha inakamilisha miradi ya maji ambayo inaendelea kutekelezwa katika maeneo tofauti nchini na kuanzisha mipya ili kukomesha kabisa tatizo la maji.

"Lakini tutahakikisha vijiji vyote vinavyozunguka miradi mikubwa ya maji vinanufaika na miradi hiyo kwa kupatiwa huduma ya maji ya bomba, tunataka kuhakikisha tunamaliza kabisa tatizo la maji nchini," alisema Samia.

Katika hatua nyingine alisema serikali itahakikisha inakamilisha ujenzi wa barabara mbalimbali katika Mkoa wa Mbeya kwa kiwango cha lami ikiwamo barabara ya Chunya – Makongolosi na Mbalizi – Galula na Mbambo - Tukuyu ili kuwarahisishia wananchi usafiri na usafirishaji.

Alisema serikali itapanua barabara kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam), kuanzia mkoani Mbeya mpaka katika Mji wa Tunduma mkoani Songwe yenye urefu wa zaidi ya kilomita 100 ili kupunguza msongamano wa magari.

Vilevile alisema ili kukabiliana na tatizo la ajira nchini, serikali itawapora viwanda watu wote waliobinafsishiwa na kushindwa kuviendeleza na watawapatia wenye uwezo wa kuviendesha ili vijana wasiokuwa na ajira waajiriwe.

"Tutafufua viwanda vyote ambavyo havifanyi kazi ili vijana wetu ambao hawana ajira waajiriwe wakafanye kazi huko na waendeshe maisha yao na walipe kodi," alisema Samia.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, alisema kwa sasa chama hicho kinakubalika kuliko ilivyokuwa mwaka 2015 na kwamba wanakusudia kulikomboa Jimbo la Mbeya Mjini ambalo kwa miaka 10 linaongozwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Alisema wananchi wa Jiji hilo wameahidi kukipigia chama hicho kura nyingi kwa sababu wamekosa maendeleo kwa muda mrefu.

"Mnavyotutembelea mara kwa mara mnazidi kutuimarisha zaidi, chama chetu kwa sasa kinakubalika zaidi na ndiyo maana wanakuwa wengi kwenye mikutano yetu," alisema Mwakasole.

Mgombea ubunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, aliwaomba wananchi wa jiji hilo kumwamini yeye pamoja na wagombea udiwani wa kata zote ili chama hicho kiunde halmashauri.

Alisema ana wadau wengi wa maendeleo ambao endapo atashinda atawashawishi waende wakashirikiane naye kuwapelekea wananchi maendeleo.



# Mwinyi kuondoa usumbufu kodi kwa wafanyabiashara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MGOMBEA wa urais wa Zanzibar kupitia CCM, Dk. Hussein Mwinyi, amesema mfumo wa kuwapatia vitambulisho vya matumizi ya mwaka mmoja wafanya biashara wadogo utasaidia kuwaendeleza na kuondoa usumbufu wa kulipa ushuru kila siku katika maeneo yao ya biashara.

Dk. Hussein alisema hayo alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara na wajasiriamali katika soko la Kinyasini na soko la Mamalishe Kinyasini, Mkoa wa Kaskazini Unguja, akiwa katika kampeni za kisayansi za kukutana na makundi maalum kuzungumzia malengo yake ya kuleta maendeleo katika sekta ya biashara hasa kwa wafanyabiashara wadogo.

Alisema badala ya mfanyabiashara kulipa ushuru wa Sh. 720,000 kwa mwaka, utaratibu wa kuwapatia vitambulisho vya biashara kwa gharama ya Sh. 30,000 utawasaidia kuokoa zaidi ya Sh. 690,000 jambo ambalo litasaidia kuongeza mitaji na kipato chao.

"Jambo la kufurahisha ninazo taarifa kwamba mchakato wa kuwapatia vitambulisho vya biashara kwa gharama nafuu na kulipia kwa mwaka umeanza kufanyika na serikali ijayo kazi yake itakua kuliendeleza hilo ndiyo maana nasema yajayo ni neema tupu na yanafurahisha," alisema.

Akizungumzia maendeleo ya wajasiriamali katika sekta ya biashara alisema kuanzia sasa waanze kuunda vikundi wakiwamo mamalishe ili waweze kunufaika na mikopo ya gharama nafuu pamoja na mfuko wa kuendeleza wajasiriamali, jambo ambalo litawasaidia kuongeza mitaji kwa biashara wanazofanya.

Alisema serikali ijayo imelenga kutumia sekta isiyo rasmi kuongeza ajira kwa kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara na kuwawezesha mitaji ili wajasiriamali waweze kuzalisha bidhaa bora na kuyatumia masoko ya ndani na nje.

Kuhusu changamoto ya kukosekana huduma ya maji na vyoo katika soko la mamalishe Kinyasini, alisema mambo hayo yatafanyiwa kazi, ili kuhakikisha masoko yote yanaendesha biashara yakiwa katika mazingira mazuri, lakini Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, Nadil Abdlatif na mgombea ubunge katika jimbo hilo waliahidi kushughulikia changamoto hizo baada ya uchaguzi mkuu.

Akizungumza na wafanyabiashara katika soko la kukausha dangaa Fungu Refu, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Dk. Mwinyi alisema lengo la serikali kuwaingiza wakaushaji wa dagaa katika matumizi ya teknolojia ya kisasa ya kukausha dagaa kwa kutumia vifaa vya kisasa badala ya mionzi ya jua.

Alisema eneo hilo sasa tayari limetengwa kwa kuanzisha kiwanda maalum cha kukausha dagaa hatua ambayo itasaidia kuongeza thamani ya bidhaa inayozalishwa pamoja na kuongeza masoko ya nje na ndani ya nchi.

Alisema viwango vya bei vitaongezeka iwapo mfumo wa ukaushaji wa dagaa utazingatia viwango vya ubora na kutaka wajasiriamali katika biashara hiyo kujiandaa na mabadiliko ya kisasa yanayotarajiwa kutokea katika kuendeleza biashara ya dagaa wa kukausha Zanzibar.

Kwa upande wao wafanyabiashara wa dagaa walisema hivi sasa wanakabiliwa na uhaba wa masoko na kutegemea soko la DRC Kongo na hivyo kukosekana ushindani wa bei na kulazimika kuuza kwa bei ndogo.

Pia, walisema wakati umefika serikali kuwajengea kituo cha polisi katika eneo hilo, pamoja na mazingira yao kuimarishwa ikiwamo barabara na upatikanaji wa huduma nyingine muhimu ikiwamo maji na umeme.



Mgombea ubunge Jimbo la Mpendae, Taufiq Salum Turky, akizungumza na waandishi wa habari jimboni humo juzi, baada ya kuchukua fomu ya kugombea nafasi hiyo, kutokana na aliyekuwa mgombea wa jimbo hilo, ambaye ni baba yake, Salum Turky kufariki dunia. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Ashikiliwa tuhuma za kusafirisha karafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Zanzibar linamshikilia Ramadhan Moh'd Ali (26), kwa tuhuma za kuhifadhi kiwango kikubwa cha karafuu ndani ya nyumba yake na kusafirisha bila kibali kutoka mamlaka husika.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Awadhi Haji Juma, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa.

Alisema mtuhumiwa huyo alikutwa na karafuu kavu magunia manane yenye uzito wa kilogramu 492.5 nyumbani kwake Kwarara, Mkoa wa Mjini Magharib Unguja alikozihifadhi.

Alisema mtuhumiwa huyo alipohojiwa alisema kuwa karafuu hizo alizitoa Kijiji cha Kinyasini, Mkoa wa Kaskazini Unguja na kuzisafirisha hadi nyumbani kwake bila ya kuwa na kibali kutoka mamlaka husika jambo ambalo ni kosa kisheria.

"Upelelezi wa shauri hili unaendelea na utakapokamilika atafikishwa mahakamani," alisema.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano wa kufichua vitendo vya uhalifu na wahalifu ili kuwachukulia hatua.

# Spika awaasa wananchi kujihadhari matapeli kisiasa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SPIKA wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, amewataka wananchi wa Jimbo la Kwahani, Mjini Unguja, kutokubali kulaghaiwa na matapeli wa kisiasa ambao hawana dhamira njema na nchi yao katika kuleta maendeleo na kutunza amani ya nchi.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa kampeni Jimbo la Kwahani na kuwanadi wagombea wa nafasi ya ubunge, uwakilishi na udiwani, mkutano uliofanyika katika uwanja wa ofisi za Jimbo Kijangwani.

Alisema wapo wanasiasa wanaowadanganya wananchi na kusema uongo kwa kutaka kura katika kipindi hiki cha kampeni na sio kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

"Wapo wanasiasa wanaowadanganya wapigakura wao hakikisheni mnafanya maamuzi sahihi kwa chama chetu ili tuendelee kuijenga nchi yetu katika kuleta maendeleo," alisema.

Alisema imefika wakati kwa wananchi kufanya maamuzi sahihi kuichagua CCM kutokana na sera zake ambazo wakati wote zimekuwa zikisisitiza suala la amani na utulivu katika nchi.

Spika Zubeir ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, alisema wananchi wafahamu kuwa amani ndiyo kila kitu katika nchi na ndio lulu kwa taifa la Tanzania.

Alisema kuwa wananchi wanapaswa kuzingatia sera za CCM, ili kufanya maamuzi sahihi kwa kukirejesha chama hicho madarakani ili kiendelee na hatua za maendeleo zilizofikiwa kutokana na utulivu uliopo.

"Jimbo la Kwahani lina historia kwa CCM kwani ndio lililotutolea mgombea wa urais wa Zanzibar, hivyo tunaamini wananchi hawatatuangusha, katika miaka mitano iliyopita tumeweza kutekeleza ilani yetu ya 2015/2020 kwa kiwango kikubwa," alisema.

Aliwaomba wanaCCM na wananchi kujitokeza kwa wingi siku ya Oktoba 28, ili kukiwezesha chama chao kuendelea kushika dola.

Aliviomba vyama vingine vya siasa kuhubiri amani wakati wote katika mikutano yao kwa kuwa kutofanya hivyo kunaweza kuharibu amani iliyopo.

Akizungumza kwa niaba ya wagombea wenzake, mgombea ubunge wa jimbo hilo, Ahmada Yahya Abdul- Wakil, aliahidi kuwaletea maendeleo wananchi wa jimbo hilo kwa kushirikiana na viongozi wengine wa jimbo hilo endapo atashinda katika uchaguzi mkuu.

Alisema, serikali kupitia Mfuko wa Halifa Found, imetenga Sh. bilioni 20 kwa ajili ya vijana kujiendeleza kiuchumi na kujipatia maendeleo kupitia miradi mbalimbali.

"Naahidi kwa kushirikiana na viongozi wenzangu wa jimbo hilo kujenga kituo cha ujasiriamali cha kisasa katika jimbo hilo ili kuwawezesha vijana kuzalisha bidhaa mbalimbali na kuuza na eneo tayari lipo," alisema.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- Kuboresha biashara
- Kulipa kodi ya nyumba
- Kumalizia tenda
- Kulipa matibabu n.k.

Mawasiliano yetu: Dar es salaam **– 0768 928 516. Arusha – 0677 226 960.**

### VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa eneo la Mkundi/Banana mtaa wa bwawani -Morogoro. Ina vyumba vinne self container, sebule, dining room na choo cha nje ndani ya fensi. Wasiliana na simu 0713-435172/0713-440436.

### VIWANJA/MASHAMBA

**ENEO LINAUZWA,** Eneo linauzwa Makongo juu Dar-es-salaam karibu na Petrol Station mwisho wa lami Lina Nyumba nne za kuishi, umeme, maji ya kisima na dawasco ipo ndani ya fensi. Wasiliana na simu: 0753-029141/0779-999041.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA CHETI



**MAGDALENA REVOCATUS SHIRATI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.314/0051** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KAZIMA SEKONDARI** mwaka 1996. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KAWE/RB/4951/2020.**

115913302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;275/2020**

**Ombi la PENDO JOELY CHAMBO., Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu TATU ALLY WAIKELA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 16/10/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/09/2020.

Tarehe 16/9/2020

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

115911802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S. M. M 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo ARUSHA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi 268 2020**

**Ombi la ZEPHANIA SAITABAU ABRAHAM Msimamizi wa mirathi marehemu EMMANUEL PAULO LOMNYAKI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 19-10-2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 16-09-2020

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
ARUSHA MJINI

115913602

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 51 OF 2020**
**In the matter of the estate of the late JOHN JACOB KIBWANA of MAILI MBILI within Dodoma city council**
**And**
**In the matter of Application for letters of administration by PATRICIA MAGANGA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claimed to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 09 day of October 2020.

Dated at 17 this day of 8/2020
OR
PETITIONER

Presented for filing this 16th day of Sept 2020

RESIDENT MAGISTRATE

**DRAWN AND FILED BY:**
**THE PETITIONER**
**MAILI MBILI**
**CHAMWINO WARD**
**DODOMA REGION**

115913702

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF BUKOBA AT BUKOBA**

**CIVIL CASE NO. 10 OF 2015**

**1. NICKSON NELSON SAMSON @ NDYAMUKAMA..................PLAINTIFF**
**2. JONSTON JOAS ..........................PLAINTIFF**
**3. AGNES GODFREY ..........................PLAINTIFF**
**4. SIMON GERVASE ..........................PLAINTIFF**
**5. ODILO OSWARD ..........................PLAINTIFF**
**6. JESCA DOMICIAN ..........................PLAINTIFF**
**7. NEEMA JOHN ..........................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**CHINA HENAN INTERNATIONAL COOPERATION GROUP (CHICO)..........................1ST DEFENDANT**
**CHICO–CRSG JOINT VENTURE ..........................2ND DEFENDANT**
**SUMMONS TO APPEAR AND FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE**
**(O.V,r 1 CPC)**

**TO: CHICO – CRSG JOINT VENTURE**
WHEREAS the above named Applicant(s) has/have instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint;
**Y**
**OU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within twenty one (21) days of service of this notice upon you. If there is more than one plaintiff, additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the Plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not joint defence, you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.

**AND TAKE NOTICE** that if you default in filing the written statement of defence within the time specified, the court may pronounce judgment against you.

**TAKE FURTHER NOTICE** that the case also has been fixed for order before Hon. W. YONA – RM Magistrate on the28th day of SEPTEMBER, 2020 at 08:30 O'clock in the forenoon/afternoon.

GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT 10TH Day of SEPTEMBER, 2020

RESIDENT MAGISTRATE
BUKOBA

DEFENDANT

215914102

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KILIMANJARO GOLF DEVELOPMENT LIMITED** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T 588 ASJ TOYOTA LAND CRUISER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/683054/2020.**

115912002


***Uza,***

***Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza***

***Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# China, Marekani zavutana kuenea corona

**BEIJING,** China

MVUTANO kati ya Marekani na China umejitokeza katika mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa mjini New York, baada ya Rais wa Marekani Donald Trump kulaumu China kwa kueneza virusi vya corona.

Rais Trump ameitaka China iwajibishwe kutokana na janga la corona.

Kati hotuba yake, Rais wa China Xi Jinping alisema nchi yake haina nia ya kuingia katika vita baridi na nchi yoyote.

Uhusiano kati ya nchi hizo mbili zenye uwezo umezorota katika nyanja tofauti.

Mkutano wa mwaka huu mjini New York unaendeshwa zaidi kupitia mfumo wa kidijitali, huku viongozi wa duniani wakiwasilisha hotuba zilizorekodiwa.

Mfumo huo mpya ulimaanisha sarakasi za siasa za kimataifa zinazoshuhudiwa katika mkutano huo hazikuwapo.

**Katika siku za mwanzo za virusi, China ilisitisha safari za ndege za ndani, huku ikiruhusu ndege kuondoka China na kuambukiza ulimwengu.**

Kila nchi iliwakilishwa na mjumbe mmoja na kulikuwa na nafasi ndogo kwa nchi kujibizana.

Kama ilivyotarajiwa, Rais Trump alitumia hotuba yake kushambulia mahasimu wake na kusema, "Lazima tuwajibishe nchi ambayo ilileta pigo hili kwa ulimwengu, China," alisema.

"Katika siku za mwanzo za virusi, China ilisitisha safari za ndege za ndani, huku ikiruhusu ndege kuondoka China na kuambukiza ulimwengu.

"China ililaani marufuku yangu ya usafiri dhidi ya nchi yao, licha ya kwamba walifutilia mbali safari za ndege za ndani na kuwafungia raia wake majumbani."

Rais Trump ambaye rekodi yake kuhusu virusi vya corona inachunguzwa kwa makini wakati nchi hiyo inapoelekea katika uchaguzi, mara kwa mara amekuwa akilaumu Beijing kwa kuficha ukweli kuhusu virusi hivyo, akisema wangesaidia kuzuia kusambaa kwa corona.

China imetaja tamko hilo kuwa uzushi usiokuwa na msingi wowote.

Idadi ya vifo vya corona nchini Marekani imefikia zaidi ya watu 200,000, ambayo ni ya juu zaidi duniani japo Rais Trump amekuwa akipuuza ugonjwa huo.Hali ya taharuki imekuwa ikiongezeka kati ya Marekani na China katika masuala tofauti, ikiwamo biashara, teknolojia. Akizungumza muda mfupi baada ya kiongozi wa Marekani, Rais Xi alionya kuhusu hatari ya mgongano wa ustaarabu.

"Tutaendelea kushughulikia tofauti na kutatua mzozo kati yetu na wengine kupitia majadiliano, kamwe hatutaanzisha mchezo ambao hauna manufaa," alisema.

Katika tamko lake lililotolewa kabla ya hotuba yake ya Jumanne, Rais Xi alitumia mbinu ya ustaarabu kushambulia Marekani, akisema hakuna nchi ina haki ya kusimamia masuala ya kimataifa, kuamua hatima ya wengine, ama kutumia manufaa yaliyopatikana kujiendeleza."

Pia katika hotuba yake, Rais Xi alisema China ndiyo taifa kubwa duniani linalokuza gesi safi na lengo lake ni kukomesha utoaji wa gesi chafu ifikapo mwaka 2030.

Mkutano huo ulifunguliwa rasmi na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ambaye bila kutaja China au Marekani alisema lazima wafanye kila wanaloweza kuepusha vita baridi. **BBC**



Kuanzia sasa raia wa Kenya watashiriki shughuli za mazishi ya wapendwa wao waliofariki kwa corona baada ya serikali kulegeza masharti tofauti na awali ilipiga marufuku. **PICHA: EPA**

## Afrika 'yapewa tano' vita corona

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

MKUU wa Kituo cha Kudhibiti Magonjwa Afrika (CDC), John Nkengasong, amewasifu viongozi wa Afrika kwa kuunga mkono jitihada za pamoja za kushughulikia janga la virusi vya corona.

Nkengasong aliiambia BBC kuwa, mkakati wa afya ya umma barani Afrika, ukiwamo wa ongezeko la upimaji, kuwafikia wale waliohusiana na walipata corona pamoja na uvaaji wa barakoa umeweza kushusha kiwango cha maambukizi.

Shirika la Afya Duniani (WHO) awali lilisema kuwa mlipuko wa corona barani Afrika unaweza kuwa makubwa zaidi.

Jumatatu, takwimu mpya zimeonyesha kuwa virusi vipya vya corona vimeshuka kwa asilimia 12 barani Afrika.

Dk. Nkengasong alisema takwimu zinawakilisha jitihada za kiafya za umma na viongozi wa bara zima kwa ujumla katika kulinda afya.

Alisema virusi hivyo katika jumuiya hiyo vilihitaji umoja katika kupambana dhidi ya janga hilo na hicho ndicho kilichofanyika. **BBC**

## Mpinzani Zimbabwe azuiwa mitandaoni

**HARARE,** Zimbabwe

MWANASIASA wa upinzani nchini Zimbabwe, Job Sikhala, ameachiwa kwa dhamana baada ya kuwekwa mbaroni mwezi uliopita akihusishwa na maandamano dhidi ya serikali.

Sikhala alikamatwa na polisi Agosti 21 na kushtakiwa kwa kosa la uchochezi na uhamasishaji wa vurugu baada ya maandamano yaliyotokea Julai 31.

Sikhala ameachiwa huru juzi baada ya kutoa dhamana ya dola za Marekani 590 na kupewa amri ya kutoweka ujumbe wowote mtandaoni na kwenye makundi ya WhatsApp.

Chama chake cha Movement for Democratic Change kiliandika hayo kwenye kurasa ya tweeter. **BBC**

## Bunge laamua hatima ya uchaguzi mkuu Ethiopia

**ADDIS ABABA,** Ethiopia

BUNGE la Ethiopia limepitisha azimio la kuruhusu taifa hilo kuahirisha uchaguzi mkuu na kutaka ufanyike ndani ya mwaka mmoja.

Mwaka mpya wa Ethiopia unaanza Septemba 11, hivyo uchaguzi utafanyika kabla ya mwezi Septemba mwaka huu.

Bunge limepitisha azimio hilo katika kikao maalum kilichofanyika Jumanne.

Mbunge mmoja alipiga kura kupinga azimio hilo wakati nane waliridhia, kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Ethiopia.

Taifa hilo limeahirisha uchaguzi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Waziri Mkuu wa nchi hiyo, Abiy Ahmed, alisema ikiwa ukanda wa Kaskazini wa Tigray ukiendelea na uchaguzi basi utatambulika kuwa batili.

Chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF) kilishinda kwa kura za asilimia 98 katika uchaguzi wa kikanda.

Kiongozi wake, Debretsion Gebremichael, alitaja uchaguzi huo kuwa wa kihistoria. **BBC**

## Navalny aruhusiwa kutoka hospitalini

**MOSCOW,** Urusi

KIONGOZI wa upinzani wa Urusi, Alexei Navalny (44), ambaye mataifa ya Magharibi yanaamini alipewa sumu inayoathiri mishipa ya fahamu ya Novichok, ameruhusiwa kutoka hospitali baada ya kukaa kwa mwezi mmoja.

Viongozi wa Ulaya wametaka maelezo kutoka serikali ya Urusi tangu Navalny alipougua baada ya kusafiri kwa ndege kutoka Siberia mwezi Agosti na alifikishwa hospitalini kabla ya kusafirishwa hadi Berlin kwa matibabu zaidi.

Hospitali hiyo ilisema kuwa mkosoaji huyo mkubwa wa serikali ya Urusi na mwanaharakati wa kupinga rushwa alikaa kwa siku 32 katika hospitali ya Charitte katika mji mkuu wa Ujerumani, Berlin ikiwa ni pamoja na siku 24 katika chumba cha wagonjwa mahututi, kabla ya kuruhusiwa jana. **DW**



# SHAW AITAKA UNITED KUSAJILI NYOTA WAPYA

**MANCHESTER,** England

MLINZI wa kushoto wa Manchester United, Luke Shaw ameitaka bodi ya wakurugenzi ya klabu hiyo, kununua wachezaji zaidi baada ya kikosi chao kuchapwa mabao 3-1 na Crystal Palace kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu England.

United imemsajili Donny van de Beek pekee, ambaye alicheza Jumamosi mechi yake ya kwanza na kufunga bao hilo.

Shaw anaamini kushindwa kufanya usajili kutawafanya waachwe mbali na wapinzani wao kwenye Ligi Kuu England, ambao wameboresha vikosi vyao.

Shaw alisema: "Tuna kundi zuri sana la wachezaji, lakini binafsi nadhani tunahitaji kuboresha kikosi chetu."

Beki huyo alisema kitendo cha kushindwa kucheza mechi za maandalizi ya msimu mpya, kimeonekana kuwa na madhara makubwa kwa timu hiyo wakati wa mchezo wao huo, ambapo mastaa wa Man United walipumzika kwa siku 34 tu tangu walipochapwa kwenye nusu fainali ya Europa League dhidi ya Sevilla.



# Werner: Chelsea haiwezi kubeba EPL msimu huu

**LONDON,** England

TIMO Werner amesema, Chelsea haiwezi kubeba ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu licha ya kutumia pauni milioni 210 kusajili wachezaji wapya.

Werner alitua Chelsea akinaswa kutoka RB Leipzig, kwa ada ya pauni milioni 48, huku nyota wengine walionaswa wakiwa ni Kai Havertz kwa pauni milioni 70, Ben Chilwell kwa pauni milioni 50 na Hakim Ziyech pauni milioni 36.

Kocha wa The Blues hao, Frank Lampard alimnasa pia beki wa kati Thiago Silva kwa uhamisho huru kutoka Paris Saint-Germain, lakini akilipwa mshahara mkubwa.

Werner, ambaye alifunga mabao 36 kwenye Bundesliga msimu uliopita akiwa na kikosi cha RB Leipzig, anadhani Chelsea mpango wake haoni kama utakuwa tayari na kuchuana kwenye mbio za ubingwa msimu huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 24, ameliambia gazeti la Bild: "Lazima tuwe wakweli na kwa kusema hilo hatuwezi kushinda Ligi Kuu England, wala Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

"Kama itafanikiwa, basi litakuwa jambo zuri. Lakini, hilo si ambacho klabu inatarajia. Nataka kuwalinganisha na Liverpool kwa miaka michache iliyopita.

"Kwa mipango yetu Chelsea, tunataka kuboresha mambo hatua kwa hatua kufikia malengo ya kubeba ubingwa katika kila msimu."

# Barca hawataki Suarez ajiunge Atletico Madrid

**BARCELONA,** Hispania

LUIS Suarez na Barcelona wamekubaliana kuachana kwa amani baada ya mpachika mabao huyo wa Uruguay, kuelezwa bayana kuwa hayumo kwenye mipango ya kocha mpya, Ronald Koeman.

Awali, Suarez alikuwa na mpango wa kuungana na Cristiano Ronaldo kule Juventus, lakini dili hilo limeshindikana baada ya kocha, Andre Pirlo kuelekeza macho yake kwa straika wa Atletico Madrid, Alvaro Morata.

Hata hivyo, Barcelona imeibuka na kueleza kuwa Suarez ataruhusiwa kuondoka bure, lakini kuna klabu nne ambazo hatatakiwa kwenda kujiunga nazo.

Miongoni mwa klabu hizo ni Atletico Madrid, Real Madrid, PSG na Manchester City.

Kwa mujibu wa Onda Cero, imeelezwa kuwa awali Atletico Madrid haikuwa kwenye klabu, ambazo hazitakuwa na nafasi ya kumnasa Suarez bure, lakini kwa sasa wanafikiria kuweka kiwazo hicho.

Hofu kubwa ya Barcelona kuweka vikwazo kwa Suarez kutua kwenye klabu hizo ni kwamba, wanaweza kukutana naye kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ama La Liga kisha akawafunga, jambo ambalo hawataki litokee.



# SMALLING BADO BEI JUU SOKONI



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ameelezea kwamba, Chris Smalling bado yupo kwenye klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England kwa sababu hakuna klabu iliyofikia bei yake.

Smalling aliachwa katika kikosi cha United kilichoifunga Luton Town 3-0 kwenye raundi ya tatu ya Kombe la EFL, Jumanne. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, alikuwa na kiwango cha kuvutia wakati akicheza kwa mkopo kule AS Roma, msimu uliopita na miamba hao wa Serie A wanataka kumsajili moja kwa moja Smalling.

Lakini, Man United inataka kiasi cha pauni milioni 18 kama ada ya kumuuza mlinzi huyo, huku Roma wakionekana kutoafiki kiasi hicho cha fedha.

"Kwa wakati huu, hatujapata ofa yoyote ambayo tunaitaka," alisema Solskjaer baada ya mchezo wa juzi pale kwenye Uwanja wa Kenilworth Road.

"Hiyo ndio hali halisi." "Kwamba thamani ya Smalling ipo juu. Mimi si mtu ninayefanya majadiliano ya makubaliano kati ya klabu hizi mbili, lakini hatujaridhika na kiwango kinachotakiwa kutolewa."

# Henderson afurahia kutimiza ndoto Utd

**LUTON,** England

DEAN Henderson amefurahia kutimiza ndoto yake ya kuidakia Manchester United kwa mara ya kwanza wakati akiisaidia kutinga raundi ya nne ya Kombe la Carabao baada ya kuichapa Luton.

Henderson aliokoa mchomo wa hatari wa Tom Lockyer, ambao kama angezembea basi lingekuwa bao la kusawazisha kwa Luton baada ya kutanguliwa kwa bao la Juan Mata aliyefunga kwa mkwaju wa penalti dakika ya 44.

Mabao mengine mawili kutoka kwa Marcus Rashford na Mason Greenwood yaliifanya Manchester United kwenye mchezo huo kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 wakiwa ugenini.


"Nilikuwa nikiota hili maisha yangu yote," Henderson aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

"Nashindwa kuamini kucheza mchezo wangu wa kwanza kwa klabu ninayoipenda," ujumbe huo uliendelea kueleza hisia zake.

Henderson ni zao la akademi ya Manchester United, lakini amekuwa akiishia kucheza kwa mkopo na misimu miwili iliyopita alikuwa akiichezea Sheffield United.

Kipa huyo msimu uliopita ulikuwa na neema kwake kwani ulimfanya kupata nafasi ya kuitwa kwa mara ya kwanza katika kikosi cha timu yake ya Taifa ya England 'Three Lions'.

Ubora wake unatajwa kuwa utakoleza vita ya namba kwenye kikosi cha Manchester United, ambacho kimekuwa kikimtegemea David de Gea kama mlinda lango wao namba moja.






# *England bado yazuia mashabiki uwanjani*

**LONDON,** England

WAZIRI Mkuu wa England, Boris Johnson, amethibitisha kuwa mpango wa kuwarudisha mashabiki viwanjani kushuhudia matukio ya kimichezo nchini humo, kuanzia Oktoba Mosi hautawezekana.

Inaelezwa kuwa mpango huo umetupiliwa mbali baada ya idadi ya wachezaji na viongozi wanaopimwa na kukutwa na virusi vya corona kuongezeka.

"Tumetambua kuwa maambukizi yameongezeka maradufu na tumeamua kusogeza mbele," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

Akizungumza na vyombo vya habari nchini humo, Boris amesema wataongeza vizuizi zaidi katika kujikinga na virusi vya corona ikiwamo kuzuia mashabiki kujitokeza viwanjani.

"Hatutaweza kuruhusu mashabiki kuanzia Oktoba Mosi, tunajua athari ambazo zinaweza kujitokeza, endapo mashabiki wataanza kuingia viwanjani," aliongeza.

Michezo mingi mikubwa nchini England imekuwa ikiendelea, bila uwapo wa mashabiki kutokana na janga la virusi vya corona tangu Machi 13, mwaka huu.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TORREIRA CHAMBO YA PARTEY ARSENAL

## ● ● ● Ni baada ya Atletico kumkataa Lacazette na kuonyesha nia kwa kiungo huyo, sasa Arteta...

**LONDON,** England

ARSENAL inataka kumtumia kiungo wake kutoka Uruguay, Lucas Torreira, ili kufanikisha mchakato wa kuinasa saini ya kiungo wa Atletico Madrid na timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey katika dirisha hili.

Arsenal inataka kumtoa Torreira, ili kukwepa kutoa kiasi kikubwa cha pesa, ambacho kipo kwenye mkataba wa Partey.

**Hii ni mara ya pili kwa miamba hiyo kujaribu kufanya hivyo baada ya mara ya kwanza kumtumia Alexandre Lacazette, lakini Atletico ilikataa na kusisitiza kuwa inahitaji pesa na si mabadilishano ya wachezaji.**

Torreira mwenye umri wa miaka 24, amekuwa hapati nafasi ya kucheza katika kikosi cha kwanza cha Arsenal tangu Kocha Mikel Arteta achukue rasmi kibarua cha kuinoa miamba hiyo, hivyo Arsenal imekuwa ikijaribu kumuuza, ili kusajili mchezaji mwingine ambaye atakuwa chaguo la kocha.

Usajili wa Partey unaweza kuwa bora zaidi Arsenal kutokana na kiwango chake msimu uliopita.

## ZISIKUPITE

### UNITED KWA DEMBELE

MANCHESTER United wako kwenye mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 23, kutoka Barcelona. ***(Daily Record)***

### DELE KUTUA PSG

PARIS St-Germain wana uhakika kwamba kiungo wa Tottenham Hotspur na England, Dele Alli mwenye umri wa miaka 24, anataka kujiunga na klabu hiyo kwa mkopo wa msimu mzima. ***(Mail)***

### MAX KUJIUNGA BARCA

MLINZI wa Norwich City, Max Aarons mwenye umri wa miaka 20, amekubali mkataba wa miaka mitano kujiunga na Barcelona. (Sport - in Spanish)

### MATTEO KUONDOKA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal na Ufaransa, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 21, ameomba kuondoka klabuni hapo. ***(Tribal Football)***

### SANCHO KUBAKI DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund ina uhakika winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, hataondoka klabuni hapo msimu huu wa usajili, licha ya kuhusishwa na Manchester United. ***(Independent)***

### MILIK KUTUA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United inataka kumsajili mshambuliaji wa Napoli na Poland, Arkadiusz Milik mwenye umri wa miaka 26. (Corriere dello Sport)

### DAVIES ANUKIA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati raia wa England, Tom Davies kutoka Everton. ***(Talksport)***

### ARSENAL VITANI KWA AOUAR

ARSENAL imepata mpinzani katika mbio zake za kumwania kiungo wa Lyon na Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

### ROMERO KUSEPA UNITED

GOLIKIPA wa Argentina, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, anataka kuondoka Manchester United. ***(Sun)***

### RUDIGER NJIAPANDA CHELSEA

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 27, anaangalia hatima yake klabuni hapo baada ya kuachwa kwenye kikosi cha kwanza. ***(Sky Sports)***

### TAHA HATAKIWI LEICESTER

MLINZI wa Bayer Leverkusen, Jonathan Tah mwenye umri wa miaka 24, hayuko kwenye orodha muhimu ya wachezaji wanaowaniwa na Leicester City. ***(Kicker)***

### UPAMECANO AITESA UNITED

KLABU ya Manchester United inania pia ya kumsajili mlinzi wa RB Leipzig na Ufaransa, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 21. ***(Telegraph)***

### BREWSTER APOTEZEWA PALACE

KLABU ya Crystal Palace imekana kutoa ofa ya pauni milioni 25 kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji kinda wa Liverpool na timu ya Taifa ya Vijana ya England chini ya miaka 21, Rhian Brewster, 20. ***(Goal)***

### EVERTON, ARIAS WATETA

EVERTON ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mlinzi wa Atletico Madrid na Colombia, Santiago Arias mwenye umri wa miaka 28. ***(Liverpool Echo)***

## Mshindi promosheni ya TIGO apatikana

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Zanzibar, Ally Bangeni Haji, amejishindia Sh. milioni 10 katika droo ya mwisho ya promosheni ya Tigo ya 'Soka Trivia' iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana.

Akizungumza baada ya kupigiwa simu na Mtaalamu wa Huduma za Ziada kutoka Tigo, Fabian Felician, kumfahamisha kuwa ameibuka mshindi, alisema anayofuraha kufanikiwa kuibuka mshindi katika promosheni hiyo.

"Sikutegemea kabisa kuwa ningeibuka mshindi katika promosheni hii, habari hizi naziona kama ndoto kwangu, naishukuru familia yangu na Tigo, familia yangu imenisaidia pakubwa kuweza kushiriki na hatimaye kuibuka mshindi.

"Nashukuru pia Tigo kunipa fedha hizi, kwani mimi ni mkulima na fedha hizi zitanisaidia kwa kiasi kikubwa kutatua changamoto mbalimbali hapa nyumbani," alisema.

Felician alimpongeza mshindi huyo na kutumia fursa hiyo kuwashukuru wateja wote, ambao walishiriki na baadhi yao kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo zawadi za fedha taslimu, ambazo zilitolewa na kampuni hiyo.

"Tunawashukuru wateja wetu wote walioshiriki kwenye promosheni hii ya miezi mitatu, ambayo imemalizika mwishoni mwa Agosti mwaka huu," alisema Felician.

## Tamasha muziki kufanyika Dar

**Na Faustine Feliciane**

ZAIDI ya wasanii 15 wanatarajiwa kushiriki kwenye tamasha kubwa la muziki wa asili na maonyesho ya sanaa litakalofanyika Jumamosi, jijini Dar es Salaam.

Tamasha hilo limeandaliwa na Taasisi ya Nafasi Art Space na litafanyika kwa udhamini wa Ubalozi wa Ufaransa nchini Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, mratibu wa tamasha hilo, ambaye ni Meneja wa sanaa za maonyesho wa taasisi hiyo Kwame Mchauru, alisema kuwa wasanii watakaoshiriki kwenye muziki ni wale wanaopiga muziki wao katika mtindo wa kiasili wakichanganya na vionjo vya kisasa.

"Mbali na muziki, lakini pia kutakuwa na maonyesho mengine ya vitu vya sanaa, wasanii wengi wa vitu vya asili watakuwapo na tunatarajia ratiba itaanza asubuhi hapa hapa Nafasi Art Space," alisema Mchauru.

Aidha, aliwataja baadhi ya wasanii ambao watakuwapo kutoa burudani kuwa ni Shabo Makota, Bahati Band, Wahapahapa, One the Incredible, Tara Jaza pamoja na Leo Mkanyia.

Aidha, alisema kuwa tamasha hilo limegawanywa katika sehemu mbili, ambapo kutakuwa na maonyesho ya sanaa pamoja na sanaa ya jukwaani.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo, Ushirikiano na Sanaa wa ubalozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Cecile Frobert, alisema Ubalozi wa ufaransa unaona umuhimu wa kukuza tamaduni na sanaa na ndio sababu ya kushirikiana na Nafasi Art Space kuandaa tamasha hilo.

# MUGALU ATAKA NAMBA KIKOSI CHA KWANZA

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya juzi kuifungia timu yake katika mechi ya pili mfululizo, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya African Lyon, mshambuliaji wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Mkongomani Chris Mugalu, amesema atazidi kujituma, ili aweze kumshawishi Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vandenbroeck, kumpanga kikosi cha kwanza.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam, Mugalu alifunga bao la kwanza dakika ya 47 kabla ya Charles Ilamfya kutupia la pili dakika sita baadaye, hilo likiwa ni bao la pili mfululizo ndani ya siku mbili kwa Mkongomani huyo baada ya Jumapili kutupia la nne kwenye ushindi wa 4-0, Simba iliyoupata dhidi ya Biashara United katika mechi ya Ligi Kuu Bara.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya mechi hiyo, Mugalu alisema licha ya Ligi ya Tanzania kuonekana kuwa na ushindani mkubwa, atapambania nafasi yake kwa lengo la kutimiza malengo aliyojiwekea, pamoja na kuiweka timu yake mahali pazuri.**

"Lengo langu ni kuendelea kufanya vizuri kwenye kila mchezo nitakaocheza kwa kuhakikisha naipatia goli timu yangu kwa sababu ndani ya kikosi chetu kila mchezaji anajituma, ili aweze kupata nafasi," alisema Mugalu.

Alisema ataendelea kufanya mazoezi kwa bidii huku akishirikiana na wachezaji wenzake kwa kutambua umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, huku akifuata kwa makini maelekezo ya kocha wao.

"Kikubwa ni kufuata maelekezo ya mwalimu pamoja na kushirikiana na wachezaji wenzangu, ili tuiweke timu yetu katika nafasi nzuri kuweza kutetea ubingwa wetu," alisema.

Aidha, aliwaahidi mashabiki wao kufanya vizuri msimu huu na kwamba, anajipanga kukutana na timu ya Gwambina FC ambayo watakutana nayo wikiendi hii, huku akieleza kufurahishwa na kiwango cha straika mwenzake, Mnyarwanda Meddie Kagere.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, akikabidhi mfano wa hundi kwa mshindi wa Jackpot, Lilian Laizer, mkazi wa Turiani Morogoro baada ya kushinda ubashiri wa mechi zote 13 kwa usahihi. Kulia ni mumewe Lowasa Mollel akishuhudia makabidhiano hayo yaliyofanyika kwao, Turiani Morogoro. **PICHA: SPORTPESA**

# Mshindi mil. 267/- kugeukia biashara

**Na Mwandishi Wetu**

MSHINDI wa Jackpot ya SportPesa, Lilian Ngitoria Laizer, amekabidhiwa kitita chake kiasi cha Sh. 267,800,060 na Kampuni ya Michezo na Burudani ya SportPesa Tanzania, huku akieleza mipango yake ni kufungua biashara kubwa.

Fedha hizo alizokabidhiwa jana Turiani, Morogoro na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas, ni baada ya serikali kukata kodi yake kiasi cha Sh. 53,559,612 kwa mujibu wa taratibu.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa hundi hiyo, Lilian ambaye alifunguka kuwa yeye ni shabiki mkubwa wa Klabu ya Simba na Arsenal, alisema kuwa atazitumia fedha hizo kuanzisha biashara ambazo zitamuongezea kipato.

"Mimi ni mfanyabiashara wa kuuza vitenge, sina mtaji mkubwa na biashara yangu ilikuwa kwa ajili ya kutafuta fedha ya matumizi ya kawaida tu," alisema Laizer.

Alifafanua kuwa atafanya utafiti wa kina kujua ni biashara gani ambayo ataifanya huku akifikiria kujenga nyumba na kusaidia familia yake.

Kuhusu ubashiri wake, alisema wakati akibashiri matokeo hayo, mumewe alimsaidia mechi moja tu kufikisha 13 kwa mujibu wa taratibu.

"Sikuamini baada ya kuambiwa nimeshinda kiasi kikubwa cha fedha kupitia mchezo wa kubahatisha wa SportPesa, lakini baada ya kuhakikishiwa, nilikuwa na furaha sana na kusubiri siku maalum ya makabidhiano," alisema.

Alisema kuwa amekuwa akibashiri na SportPesa mara nyingi na aliamini kuwa ipo siku atakuwa mshindi kama ilivyokuwa kwa wengine jambo ambalo limetokea.

Kwa upande wa Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba, alisema Lilian amefanikiwa kupata kiasi kikubwa cha fedha baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 13 za ligi mbalimbali za soka duniani.

"Nampongeza kwa ushindi huu, amekuwa mmoja wa washindi wetu watano wa Jackpot na wa pili kwa mwanamke kuibuka na ushindi wa kiasi kikubwa cha fedha, namshauri kutumia fedha hizo katika masuala la maendeleo," alisema Tarimba.

Tarimba alisema kuwa SportPesa imedhamiria kubadilisha maisha ya Watanzania kwa kujishindia fedha nyingi na ndiyo maana Jackpot yao imeanzia Sh. milioni 200.

"Tuna furaha kubwa kuwaongezea vipato Watanzania kupitia michezo yetu mbalimbali, unaweza kubashiri kwa mechi na kujipatia fedha,

Lakini tumeenda mbali zaidi kwani tumekuwa tukitoa zawadi za fedha kwa wanaobashiri kwa usahihi mechi 10, 11 na 12 kupitia Jackpot Bonus na kuendelea kuwawezesha Watanzania," alisema Tarimba.

Ngitoria, 28, anakuwa mwanamke wa pili kushinda Jackpot ya SportPesa baada ya Scolastika Ngwalueson ambaye alishinda Sh. 260,319,960 Septemba mwaka jana naye akibashiri kwa usahihi mechi zote13.

Michezo

Alhamisi Septemba 24, 2020

Nipashe



Torreira chambo ya Partey Arsenal UKURASA 22

# Zlatko aeleza anachokitaka Yanga, Mtibwa

## ●●● Waifuata mapema Morogoro, Molinga naye aungana na Kamusoko Zesco...

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimeondoka leo kuelekea mjini Morogoro kujiandaa kukutana na timu ya Mtibwa Sugar, mwishoni mwa wiki kwenye mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu Bara, huku Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mserbia Zlatko Krmpotic akieleza anachotamani kukiona ni kuanza kupata mabao mengi baada ya michezo yao mitatu iliyopita kuambulia bao moja moja.

**Akizungumza na gazeti hili jana jijini Dar es Salaam kocha huyo alisema jana asubuhi aliamua kuwapumzisha wachezaji wake kwa lengo la kuweka fiti zaidi na kuwapa mazoezi ya mwisho jioni kabla ya leo asubuhi kuanza msafara wao kuelekea Morogoro.**

Alisema kwa sasa anachokiangalia ni kupata mabao kwa wingi kutokana na kutoridhishwa na ushindi wa goli moja ukizingatia timu hiyo ina wachezaji wengi wazuri wenye uwezo mkubwa wa kufunga.

Zlatko alisema pamoja na kikosi hicho kuendelea kupata muunganiko taratibu, matarajio yake ni kuona mabao mengi yanaendelea kupatikana kadri wanavyoendelea kucheza mechi za ligi hiyo.

"Kikosi kipo vizuri, lakini kwa sasa ninachokiangalia ni kuhakikisha nawapa wachezaji mazoezi ambayo yatawafanya waweze kuwa na uwezo wa kufunga magoli mengi zaidi pindi tunapokuwa uwanjani," alisema Zlatco.

Kwa upande wa Makamu Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Frederick Mwakalebela, alisema anashukuru mpaka jana asubuhi wachezaji wao wote walikuwa vizuri huku kila mmoja akiwa na morali wa kupata pointi tatu kwa mara nyingine wakiwa ugenini.

"Wachezaji wote wanaendelea vizuri, kesho ( leo) alfajiri tunatarajia kuanza safari kuelekea mjini Morogoro kujiandaa kukutana na Mtibwa Sugar wikiendi hii, maandalizi kwa ajili ya safari yetu yamekamilika kwa kiasi kikubwa," alisema Mwakalebela.

Katika mchezo uliopita, Yanga ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, iliibuka na pointi tatu baada ya kushinda kwa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao, Kagera Sugar huo ukiwa ni ushindi wa pili mfululizo ikishinda kwa bao moja baada ya kuichapa Tanzania Prisons katika dimba la Mkapa jijini Dar es Salaam.

Lakini katika mechi yake ya ufunguzi wa ligi hiyo dhidi ya Mbeya City, ililazimishwa sare ya bao 1-1 katika Uwanja wa Mkapa.

**Wakati huo huo**, straika wa zamani wa Yanga, David Molinga, amejiunga na Klabu ya Zesco ya Zambia, huku Kocha Mkuu wa klabu huyo ambaye aliwahi kuinoa Yanga, George Lwandamina akiondoka.

Magazeti ya Zambia na Mitandao ya Kijamii nchini humo, yamemnukuu Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Richard Mulenga akithibitisha habari hizo. Molinga amejiunga na timu hiyo baada ya kuachwa na Yanga msimu huu, akiwa ni miongoni mwa wachezaji takriban 16 walioachwa na klabu hiyo kwa sababu mbalimbali, ikiwamo viwango kushuka na wengine kushindwa kukubaliana dau la usajili.

Hata hivyo, Mulenga hakusema kuwa straika huyo aliyesajiliwa msimu uliopita na Yanga na kupachika jumla ya mabao 11 kwenye mechi za Ligi Kuu, amejiunga kwa mkataba wa miaka mingapi.

Straika huyo aliyesajiliwa Yanga wakati timu hiyo ikinolewa na Mkongomani mwenzake, Mwinyi Zahera sasa anaungana na mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Thabani Kamusoko ambaye aliyeichezea Yanga mwaka 2015 hadi 2019 na kisha kujiunga na Zesco.

Aidha, Ofisa Mtendaji Mkuu huyo, amesema klabu hiyo inamshukuru Lwandamina kwa muda wote aloitumikia Zesco na kumtakia kila la kheri. Lwandamina alijiunga na Zesco mwaka 2018, akitokea Yanga na hata alipojiunga na Wanajangwani hao, alitoka kuifundisha Zesco.

ALIYE JUU?...



Winga wa Luton Town, Jordan Clark, akiwa ameruka angani kuucheza mpira huku akikutana na changamoto kutoka kwa kiungo wa Manchester United, Donny van de Beek kwenye mechi ya Kombe la Ligi (Carabao Cup) iliyopigwa Uwanja wa Kenilworth Road usiku wa kuamkia jana. United ilishinda 3-0 kupitia kwa Juan Mata, Marcus Rashford na Mason Greenwood. **PICHA: MTANDAO**

# Simba wafuatiliwa kwa GPS uwanjani

**Na Saada Akida**

HATIMAYE Klabu ya Simba sasa imeanza kutumia vifaa vya kisasa vya kufuatilia mienendo ya wachezaji wake jinsi wanavyowajibika uwanjani, ili kuongeza ufanisi, kinachofahamika kama GPS.

Vifaa hivyo vilianza kutumika jana kwenye Uwanja wa Azam Complex baada ya mechi kati ya timu hiyo dhidi ya African Lyon na kushinda mabao 2-0.

Hivi karibuni Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi wa klabu hiyo, Mohammed 'Mo' Dewji, aliahidi kuleta GPS pamoja na kuwekeza katika kituo cha lishe (Nutrition Center), kuwekeza kwenye kituo cha kurudishia utimamu (Recovery) na taaluma ya kuchua misuli (Massage) pamoja na wataalamu wa saikolojia.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck alisema kifaa hicho wameanza kutumia jana na itakuwa mwendelezo ili kumrahisishia kufuatilia mienendo ya wachezaji wake.

Alisema kifaa hicho kinapima kila kitu, ikiwamo kasi ya mchezaji aliyokimbia iwe kwenye mechi au mazoezi, mapigo ya moyo pamoja na jinsi gani alivyojituma anapokuwa uwanjani.

"Ni muhimu sana kwa kifaa hicho kuwapo, kwa sababu nitakuwa na taarifa zote za mchezaji wangu alivyotumika, tumeanza kutumia leo (juzi), katika mechi hii ya kirafiki ambayo ni muhimu kwangu kuwapa mazoezi wachezaji ambao hawakucheza mechi na wale ambao hawakumaliza dakika 90."

Sven alisema katika mechi hiyo amewatumia washambuliaji wawili kwa ajili ya kujaribu mifumo mbalimbali kulingana na jinsi ya mpinzani wao wanayekutana naye katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Nimewatumia Charles Ilanfya na Chri Mugalu, wamecheza vizuri pia Erasto Nyoni nimembadilisha nafasi na ameitendea haki na kucheza vizuri, kila mchezaji kucheza nafasi zaidi ya mbili inaleta ushindani mkubwa katika timu," alisema kocha huyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >